# Nipashe Jumapili

Jumapili Septemba 13, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • No. 0580337

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## Lissu ageukia mashamba waliyojimilikisha vigogo

UKURASA 2




UKURASA 9

MAKALA MAALUM

# Kwa nini watu wengi hufariki dunia usiku?

• **Madaktari**, viongozi wa dini wanena, miti yatajwa kuwa kiini cha tatizo... *Endelea ukurasa 2*



Mgombea urais wa Zanzibar kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Hussein Mwinyi, akiwapungia mkono wananchi, wafuasi na wanachama wa chama hicho, baada ya kuwasili katika uzinduzi wa kampeni za uchaguzi mkuu, kwenye Viwanja vya Demokrasia Kibanda Maiti, mjini Zanzibar jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Kishindo uzinduzi kampeni Dk. Mwinyi Zanzibar



Mgombea mwenza wa urais kwa tiketi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Salum Mwalimu, akihutubia mkutano wa kampeni za uchaguzi mkuu katika Kata ya Maore, wilayani Same, mkoani Kilimanjaro jana. **PICHA: FRANCIS DANDE**

## YALIYOMO


UKURASA WA 3

**MWAKYEMBE AGUSIA 'WAJUMBE'**

WAZIRI wa Habari, Dk. Harrison Mwakyembe, amewataka wanachama wa CCM kutambua kwamba kura za maoni zilishakwisha na...

UKURASA WA 8

**Darasa la Ndoa...**

**NAFASI YA FEDHA KWENYE NDOA**

FEDHA ni njema na mtu kuwa nayo siyo uovu wala dhambi. Nafasi anayoipa mtu katika maisha yake ndiyo itakayoamua kama ni njema...


## Mtaalam abainisha makosa siku 1,000 za lishe kwa watoto

UKURASA 3




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store



MICHEZO **SIMBA YAPALIWA NA MIWA YA MTIBWA** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Majaliwa ataja sifa kupigiwa kura 2020

**Na Mwandishi Wetu,** TANGA

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Kassim Majaliwa, amewataka wananchi kujitokeza kupiga kura Oktoba 28, mwaka huu kumchagua kiongozi mwenye uwezo wa kulinda tunu za taifa ikiwamo amani na muungano.

Alitoa rai hiyo jana alipomwombea kura mgombea urais wa chama hicho, Dk. John Magufuli, mgombea ubunge wa Tanga Mjini, Ummy Mwalimu na wagombea udiwani kwa tiketi ya CCM kwenye mkutano wa kampeni uliofanyika katika viwanja vya Tangamano jijini.

"WanaTanga bila ya kujali itikadi za vyama nipo hapa mbele yenu kwa unyenyekevu mkubwa ninawaomba ifikapo Oktoba 28, mwaka huu, tumchague Rais wetu Dk. John Pombe Magufuli ili akaendeleze miradi ya maendeleo aliyoianzisha.

"Pia ninawaomba tumchague Ummy Mwalimu katika nafasi ya ubunge katika jiji letu la Tanga pamoja na wagombea wa udiwani wa CCM," Majaliwa alisema.

Alisema wananchi wanatakiwa wamchague tena Dk. Magufuli kwa sababu ni kiongozi shupavu mwenye uwezo wa kufanya uamuzi na asiyekubali kuyumbishwa na yeyote.

Alisema kuwa Dk. Magufuli ni kiongozi mwenye kuwajali Watanzania na atakayewaruhusu waendelee kuabudu kwa uhuru na ndiyo maana hata uchaguzi umepangwa kufanyika siku ya Jumatano ili kutoa fursa kwa wananchi kutumia siku za Ijumaa, Jumamosi na Jumapili kuabudu.

Majaliwa alisema Sh. bilioni 66.8 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya kutoka Tanga hadi Pangani yenye urefu wa kilometa 50, ambayo inajengwa kwa kiwango cha lami. Alisema miradi mingine ya kimkakati inayotekelezwa katika jiji hilo ni pamoja na ujenzi wa dampo la kisasa katika eneo la Mpirani Chongoleani ambapo Sh. bilioni 8.9 zimetolewa kwa ajili ya ujenzi wa eneo la udhibiti wa taka ngumu na tayari ujenzi umekamilika.

Majaliwa alisema Sh. bilioni 1.7 zimetolewa kwa ajili ya ujenzi wa kitega uchumi kwenye stendi ya mabasi ya Jiji la Tanga. Alisema ujenzi unaendelea na upo katika hatua ya umwagaji zege katika ghorofa ya pili. Alisema katika mwaka wa fedha wa 2020/21, Halmashauri ya Jiji la Tanga imepanga kutumia Sh. bilioni 1.3 kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Mabawa-Msambweni II na barabara ya 11 na ya 12 kwa kiwango cha lami na sasa utekelezaji wake uko katika hatua za awali.

# Kishindo uzinduzi kampeni za Hussein Mwinyi Znz

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

CHAMA cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar, jana kilizindua kwa kishindo kampeni zake za uchaguzi wa mwaka huu, huku Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Dk. Ali Mohamed Shein, akimnadi Mgombea Urais wa Zanzibar, Dk. Ali Hussein Mwinyi.

Katika uzinduzi huo wa kampeni uliofanyika kwenye Viwanja vya Demokrasia Kibanda Maiti, Dk. Mwinyi aliyataja maeneo yaliyofanyiwa kazi katika ilani iliyopita kuwa ni kukua kwa pato la taifa kwa asilimia 6.8, kuongeza kwa pato la wananchi, uchumi kukua, kudhibiti kasi ya mfumko wa bei na usambazaji wa huduma za umeme.

Mengine ni utoaji wa elimu bure, huduma ya maji safi na salama zimeongezeka, matibabu bila malipo, watalii kuongezeka na ujenzi wa miundombinu ikiwamo barabara na viwanja vya ndege na ununuzi wa meli mpya.

Alisema mategemeo yake ni kuendeleza juhudi hizo za utekelezaji wa ilani, hivyo akawaomba wananchi kumpigia kura.

Dk. Mwinyi alisema kuwa, endapo akishinda katika uchaguzi mkuu, ataendeleza maendeleo ya Zanzibar na kuzienzi tunu za Mapinduzi na Muungano wa serikali mbili.

Alisema serikali yake pia itakuza utalii kwa kuongeza idadi ya watalii na kutoa fursa za ajira kwa wananchi katika sekta mbalimbali zikiwamo za biashara na uvuvi.

Alisema kuwa katika sekta ya mafuta na gesi, atahakikisha anaweka sheria na sera nzuri ili Wazanzibari kushiriki na kutokuwa watizamaji katika sekta hiyo.

"Ili kukuza uchumi, lazima uwe na umeme wa uhakika na wa gharama nafuu, hili nitalivalia njuga," Dk, Mwinyi alihidi.

Alisema ataboresha huduma za jamii ikiwamo elimu bora bila ya malipo hadi sekondari na kuongeza ufaulu wa wanafunzi na kupitia upya mitaala ya ufundi ili vijana wawe sehemu ya uchumi wa nchi.

Alisema kuwa serikali yake pia itaongeza udahili na mikopo kwa wanafunzi wanaotaka kujiunga na elimu ya juu sambamba na kuboresha zaidi huduma za afya.

Mgombea huyo pia aliahidi kuboresha huduma za maji mjini na vijijini na kukuza sekta ya viwanda ili vijana wapate ajira.

"Tuwe na viwanda vinavyotumia malighafi za Zanzibar ikiwamo karafuu na mwani," alisema na kuahidi kutengeneza ajira 300,000 katika eneo hilo.

Alisema ataweka mkazo katika kilimo cha biashara na chakula na kuhakikisha kunakuwa na viwanda vya kusindika matunda ili yasiharibike.

Dk. Mwinyi pia aliahidi kulinda amani na utulivu uliopo, kupiga vita aina zote za ubaguzi, akifafanua kuwa: "Uwajibikaji na utawala bora utazingatiwa, wale wote wasiowajibika, wezi, wala rushwa na ubadhirifu wa mali tutawashughulikia," alisema.

Pia, aliahidi kuyasaidia makundi maalum yakiwamo ya wasanii, wanamichezo na watu wenye ulemavu ili kupata haki zao na kujikwamua kimaisha.

Rais wa Zanzibar, Dk. Shein, aliwaomba wananchi kumchangua Dk, Mwinyi, akisisitiza kuwa ana sifa za kuwa Rais wa Zanzibar na ana uwezo mkubwa wa kuiongoza Zanzibar.

Alisema kuwa Dk. Mwinyi ni daktari bingwa wa maradhi ya binadamu, hivyo ana upeo wa kuona mbali na ndiyo maana CCM imemtua kugombea.

"Dk. Mwinyi ana heshima kubwa sana, ni mwaminifu sana, ni mtu asiye na madaha na mbwembwe," Dk. Shein alisifu," alisema.



Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) Taifa, Kheri James (kushoto), akimnadi mgombea ubunge wa Jimbo la Kinondoni, Tarimba Abbas, katika mkutano wa uzinduzi wa kampeni za ubunge uliofanyika viwanja vya Biafra wilayani humo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Lissu ageukia mashamba waliyojimilikisha vigogo

**Na Romana Mallya**

MGOMBEA Urais kwa tiketi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, ameahidi kufanya mabadiliko makubwa katika mfumo wa umiliki wa ardhi nchini, akidai kubaini vigogo wengi wamejimilikisha mashamba makubwa.

Lissu alitoa ahadi hiyo jana wakati akiendelea na kampeni zake za uchaguzi mkuu wilayani Ifakara mkoani Morogoro, akiwaambia wananchi kuwa kuna vigogo nchini wamejimilisha mashamba makubwa hususan mkoani huko.

"Wakubwa hawa wametumia madaraka yao vibaya kiufisadi, wameiba ardhi ya wananchi, wananchi wanahangaika, hawana ardhi kidogo ya kulima mazao wapate chakula, maelfu ya hekta yamekaa bure kwa sababu wakubwa wameyachukua," alidai.

Lissu alisema kuwa, kubadili mfumo wa umiliki wa ardhi nchini ni agano lake na wananchi kuhakikisha wanapata ardhi siyo tu kwa kilimo, bali pia kwa ajili ya ufugaji na kumaliza migogoro kati ya makundi hayo mawili ya wakulima na wafugaji.

Alisema serikali itakayoundwa na CHADEMA, itakuwa ya haki kwa wananchi wote na itatatua kero na usumbufu uliopo.

Alisema Mkoa wa Morogoro una utajiri mkubwa hasa katika sekta ya kilimo kulinganisha na mikoa mingine nchini, akibainisha kuwa zaidi ya asilimia 70 ya sukari inazalishwa huko.

"Bonde la Kilombero mpaka Mikumi lina uwezo wa kulisha nchi hii mchele mwaka mzima, kuna matunda, samaki, hakuna zao linalolimwa nchi hii lisilostawi Morogoro.

"Mkoa wa Morogoro umefanywa shamba la bibi na watawala wa nchi, ukitokea Mvomero uende Kilosa, watoto wa nchi hii wamejichukulia 'mapande' makubwa ya ardhi, maelfu ya hekta halafu hawazitumii.

"Kama wamechukua ardhi kwa wingi kiasi hiki, watawezaje kukubali mpinzani wa CHADEMA kuongoza ili kuanika ufisadi dhidi ya mkoa huu uliofanyika?" Lissu alihoji.

Alisema agano lake kwa wananchi endapo watampa ridhaa ya kuwa Rais wa nchi, jambo la kwanza atakalolifanya ni kutaifisha hayo mashamba makubwa aliyodai yameibwa.

## TEMDO yagawa vifaa vya mamilioni

**Na Renatha Msungu,**
ARUSHA

TAASISI ya Uhandisi na Usanifu Mitambo Tanzania (TEMDO), imefanikiwa kusambaza viteketeza taka 20 vyenye thamani ya Sh. milioni 900 katika mikoa mbalimbali nchini.

Mkurugenzi wa taasisi hiyo, Profesa Frederick Kahimba, aliwaambia waandishi wa habari jijini Arusha jana kuwa, viteketeza taka wanavyotengeneza vinasaidia kuchuja kemikali za taka kabla moshi haujatoka kusambaa na kuharibu mazingira.

Profesa Kahimba alisema moshi unaotoka kwenye vifaa hivyo ni wa kawaida ambao hauna madhara kwa jamii.

Alitaja mikoa ambayo tayari wamepeleka vifaa hivyo kuwa ni Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Dar es Salaam, Pwani, Morogoro na Shinyanga, wakitarajia kusambaza pia katika mikoa mingine yote ya nchi.

Alisema matarajio yao ni kuona kila hospitali nchini inakuwa na kiteketeza taka za hospitali ili kuepusha uchafuzi wa mazingira.

"Tumejipanga kuhakikisha hivi viteketeza taka vinaenea kila mahali, tunahitaji kuona mazingira yanalindwa ndiyo maana tukabuni hivi viteketeza taka," alisema Profesa Kahimba.

Mjasiriamali Elizabeth Mkumbo alisema TEMDO inawanufaisha kwa kiwango kikubwa kutokana na kuwatengenezea mashine na miundombinu ya kuendeleza biashara zao.

Alisema awali walikuwa wakifanya biashara kwa shida kutokana na kukosa vifaa vya kufanyia kazi, lakini kwa sasa wanafanya kazi bila wasiwasi wowote.

"Tunaomba TEMDO waendelee kutupa sapoti katika kutusaidia, hapa tulipofikia ni kutokana na msaada wa TEMDO," mjasiriamali huyo alisifu.

Alisema wameunda kikundi ambacho wanatengeneza bidhaa kupitia mashine walizopewa na TEMDO na kwamba taasisi hiyo imekuwa mstari wa mbele kuwatafutia masoko.

Mhandisi Honest Lustful alisema TEMDO wanatengeneza mashine mbalimbali kwa ajili ya uzalishaji wa bidhaa, zikiwamo mashine za kukamulia mafuta, juisi na za kukatia mabati.

# Mwakyembe: Ya kura za maoni yamekwisha

**Na Thobias Mwanakatwe,**
KYELA

WAZIRI wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, amewataka wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kutambua kwamba kura za maoni zilishakwisha na kazi iliyobaki ni kusaka kura za kutosha kwa wagombea wateule wa chama kwa ngazi ya urais, ubunge na udiwani.

Juzi, katika mkutano wa hadhara wa uzinduzi wa kampeni za Jimbo la Kyela alilokuwa mbunge wake, Dk. Mwakyembe alisema huu siyo muda wa malumbano, bali kusaka ushindi wa CCM kwa nafasi zote tatu kwa udi na uvumba.

Aliwaomba wananchi kumpa kura za urais Dk. John Magufuli kama shukrani kwa miradi mikubwa mbalimbali ya ujenzi wa barabara za lami, vituo vya afya, bandari na kituo cha forodha mpakani mwa Tanzania na Malawi.

"Ukishampigia kura Rais Magufuli, piga kura yako ya pili kwa Ally Mlaghila kwa nafasi ya ubunge na tatu kwa madiwani wa CCM kukamilisha mafiga matatu ya uongozi," alisema.

Dk. Mwakyembe aliwatahadharisha wanaCCM kuamini kwamba ushindi ni dhahiri umeshapatikana kutokana na utekelezaji mzuri wa miradi iliyofanyika, bali wahakikishe wote wanakwenda kupiga kura Oktoba 28, mwaka huu.

"Ushindi haupatikani kwa wingi wa watu kuhudhuria mikutano ya kampeni, bali kwa wingi wa kura kwenye sanduku," alionya Dk. Mwakyembe.

Makamu Mwenyekiti wa CCM Taifa Tanzania Bara, Philip Mangula, alisema Wilaya ya Kyela imebadilika kimaendeleo kutokana na Dk. Mwakyembe kusimamia vyema Ilani ya Uchaguzi ya chama 2015-2020.

Mangula alisisitiza umuhimu wa kudumisha amani na utulivu wa nchi kwa kuwa ndiyo mtaji mkubwa wa kuling'arisha taifa kimaendeleo.

Mgombea Ubunge wa Kyela, Ally Mlaghila, aliwaomba wananchi wamchague, akiahidi kuwa katika kusaka maendeleo, hatalala kwa kuwa anazifahamu kero zilizoko katika jimbo hilo.

Mlaghila wakati akiomba kura kwa wananchi hao, alikuwa amepiga magoti, akiahidi kuwa akichaguliwa atakuwa mtumishi wao na siyo kiongozi.



Mgombea Ubunge Jimbo la Kigoma Mjini kwa tiketi ya Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, akIhutubia mkutano wa kampeni za uchaguzi mkuu, Kigoma Ujiji juzi. **PICHA: SAID POWA**

# Mbaroni kwa tuhuma uhalifu wa mtandao

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, linawashikilia watu tisa wakiwamo raia saba wa kigeni kwa tuhuma za uhalifu wa mtandao.

Kati yao, wawili wanatuhumiwa kujifanya maofisa wa usalama wa taifa na polisi na kutapeli Sh. milioni 35.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Kamanda wa Polisi wa Kanda hiyo, Lazaro Mambosasa, alisema watuhumiwa hao walikamatwa kupitia msako maalum uliofanywa kwa miezi miwili kuanzia Agosti.

Aliwataja raia hao na nchi walizotoka kwenye mabano kuwa ni Adewale Oyedes (Nigeria), Ibrahim Darbey, Prince Tito na Cream Elias (wote Liberia), Basube Dominic (DRC), Sibongile Arhur (Afrika Kusini) na Baljit Singh (India).

Kamanda Mambosasa alisema raia hao wenye umri kati ya miaka 28 na 46, walikamatwa katika maeneo mbalimbali jijini kwa tuhuma za utapeli na wizi kwa njia ya mtandao. "Baada ya mahojiano, watuhumiwa hawa walikiri kujipatia Sh. milioni 10 kwa njia ya udanganyifu kupitia mtandao na baadhi ya fedha hizo zilitumika kuanzisha duka la vinywaji vya pombe kali eneo la Tangi Bovu Mbezi Beach, tumevitia mbaroni, walinunua gari aina ya Toyota Mark, luninga mbili na magodoro, yote ni matokeo ya zao la uhalifu wanaoufanya," alisema.

Kamanda Mambosasa alisema watuhumiwa hao walikiri kujihusisha na wizi kwenye taasisi za kifedha na waliingia nchini kwa njia tofauti na baada ya kufika Tanzania, walikaribishwa na Watanzania.

"Wapo Watanzania ambao wamewakaribisha kama waume zao ambao wameendelea kuishi nao, lakini kipato wanachopata ni cha kupitia wizi kwenye mitandao," alisema.

Alisema watuhumiwa hao wamekiri kufanya uhalifu huo katika nchi nyingine barani Afrika ambazo walizitaja kwenye mahojiano kuwa ni Malawi, Uganda, Kenya na Afrika Kusini.

"Nitoe onyo kwa raia wa kigeni kuwa Tanzania ni nchi yenye sheria zake, tunawapenda wageni anayetaka kuja nchini milango ipo wazi kwa kufuata taratibu zote, akiwapo nchini ana jukumu la kufuata sheria za nchi.

"Watuhumiwa hawa wameingia kwa nia ya kufanya uhalifu, nchini kwao uhalifu hautakiwi, sasa wanakuja Tanzania, hakuna atakayebaki salama kwa wale wanaokuja kwa lengo la kutenda uhalifu. Walichokipanda ndicho wanachokivuna," alionya.

Kamanda Mambosasa alisema katika msako huo, pia walikamata Watanzania wawili kwa kujifanya maofisa usalama wa taifa na polisi.

Aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Patrick Tarimo (32), mkazi wa Mwenge ambaye inadaiwa amekuwa akijitambulisha kama Ofisa Usalama wa Taifa na Castory Wambura (57), mkazi wa Kibamba anayedaiwa kujifanya ni askari polisi.

"Agosti 10 mwaka huu, Tarimo alijipatia Sh. milioni 20 kutoka kwa raia wa kigeni ambaye alimkamata na kujitambulisha kuwa ni Ofisa Usalama wa Taifa na kufanikiwa kujipatia fedha hizo.

"Agosti 21, mwaka huu mtuhumiwa Wambura alitapeli kiasi cha Sh. milioni 15 kutoka kwa wafanyabiashara watano wa sokoni Kariakoo baada ya kujitambulisha ni Ofisa wa Polisi na Mamlaka ya Mapato (TRA)," alisema.

MAKALA MAALUM

# Kwanini watu wengi hufariki dunia usiku

## ■Madaktari, viongozi wa dini wanena
## ■Miti yatajwa kuwa kiini cha tatizo

Na Moses Ismail

KILA binadamu ataonja umauti! Hili halina mjadala. Lakini, umeshawahi kujiuliza 'kwanini watu wengi taarifa za misiba yao hubainisha wamefariki dunia usiku?' Ni swali la kawaida katika udadisi wa kibinadamu.

Katika kufuatilia matangazo ya vifo, bila shaka utakubaliana na mimi kwamba, mengi huwa na taarifa taarifa kuwa "...amefariki dunia usiku wa kuamkia leo", haijalishi amefia nyumbani au hospitalini.

Udadisi huu unaweza kuibua hisia ya mambo mengi ambayo kiuhalisia pengine hayahusiani kabisa na sababu za watu wengi kufariki dunia nyakati za usiku.

Zipo dhana na hadithi nyingi za mapokeo juu ya masuala ya imani za kishirikiana zinazosimuliwa katika jamii zetu za Kiafrika. Hadithi za simulizi za mambo ya wachawi wanaoroga na kuua watu usiku.

Hilo nalo pengine likakusukuma kuamini kuwa huenda watu hao hufa kwa kurogwa.

Katika kufuatilia ukweli wa hisia hizo kwamba huenda watu wanaofariki dunia usiku ni kutokana na dhana hiyo ya kuwapo kwa uchawi, mwaka 2011 nilimwuliza aliyekuwa Mnajimu Mashuhuri Afrika Mashariki, Sheik Yahya (marehemu) "kwanini watu wengi hufa usiku?"

Pengine kwa sababu ilikuwa ni asubuhi, swali langu lilionekana kumkera Sheikh Yahya niliyekutana naye katika ofisi zake, Magomeni, alinifokea na kuniuliza "wewe unataka wafe saa ngapi?", kisha akanitimua ofisini kwake.

Baada ya saa kadhaa kupita, Sheikh Yahya alitulia na kuniita ofisini kwake, akaniambia: "Sasa rafiki yangu, asubuhi yote unaleta mambo ya vifo?"

Baada ya hapo, akaniambia kwamba, kwa elimu ya unajimu, hana jibu la swali hilo, akidai kuwa kifo hutokea tu muda wa uhai wa mtu duniani unapokwisha.


Ukiachana na imani za kishirikiana, ipo dhana nyingine ya imani za kidini kuhusu sababu za vifo kwa mwanadamu.

Katika mafunzo ya imani za kidini, waumini hufundishwa kwamba mwisho wa uhai wa mwanadamu hapa duniani ni kufa, ingawa imani hizo hazitaji sababu wala muda wa mwanadamu kufa.

Tunaaminishwa kwamba wote tutakufa na kila mmoja na kifo chake na sababu zake za kifo.

Hili la mtazamo wa sababu za imani za kiroho linaonekana kukubaliwa na watu wengi niliozungumza nao katika udadisi wangu, lakini sikupata sababu mahususi "kwanini watu wengi hufa usiku?".

Kwa mfano, nilipomwuliza imamu wa msikiti mmoja jijini Dar es Salaam juu ya suala hilo, maelezo yake hayakutoa jibu la sababu za moja kwa moja, akisema: "Mwenyezi Mungu ndiye anapanga



mwanadamu aishi kwa muda gani, azaliwe saa ngapi na afe saa ngapi.

"Katika mafundisho ya Uislamu, Bwana Mtume anatuambia kulala ni sawa na kufa. Mtu anapolala usiku ni kama amekufa, hayupo tena katika maisha ya kawaida. Na ndiyo maana tunapoamka tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufufua baada ya umauti, yaani usingizi."

Vilevile, Mchungaji Noah Kiyondo anaunga mkono mtazamo huo kwamba kifo kinapangwa na Mungu akifafanua: "Uhai wa mwanadamu upo chini ya mamlaka ya Bwana, yeye ndiye mwenye kutupa uhai na maisha ya dunia kwa nyakati zake.

"Suala la kufa usiku, asubuhi, machana au jioni siyo kitu mbele za Bwana, muhimu ni mwanadamu kujiandaa kwa umauti maana yaja kama mwizi aibavyo," anasema.

Ukiachana na dhana hizo za mila na imani za kidini, kuna mtazamo wa kisayansi, hasa unaohusiana na masuala ya tiba na afya ya mwanadamu.

Dk. Festo Maduhu anayefanya kazi katika moja ya hospitali za taasisi binafsi jijini Dar es Salaam, anabainisha kile anachokiamini kisayansi vifo vingi kutokea nyakati za usiku.

Tabibu hiyo anasema katika mtazamo wa kisayansi, vifo vingi vya usiku vinatokea kwa sababu ya mabadiliko katika mfumo wa hali ya hewa kuu mbili zinazotawala mazingira ya viumbe hai ambazo ni Oksijeni na Kabonidaioksaidi.

Dk. Maduhu anasema: "Wanadamu tunaishi kwa kutegemea hewa ya Oksijeni. Hewa hii ndiyo tunayoivuta na kuingiza ndani ya miili yetu kwa kupitia pua, kisha inaingia kwenye mapafu yetu na kwenda kwenye viungo vingine vya miili yetu kuvipa uwezo wa kufanya kazi ya kuendesha uhai wetu.

"Na wakati unapovuta hewa hiyo, ndani ya miili yetu hutoka hewa ya Kaboni (Kabonidaioksaidi) ambayo tunaiita hewa chafu. Ni hewa hatari kwa maisha yetu.

"Lakini, hii Oksijeni tunayotumia nayo hutengenezwa na mimea ambayo ni miti na majani, ambayo nayo huishi kwa kuvuta hewa ya Kaboni mchana kutwa na inapofika usiku, hubadilika na kuanza kuvuta hewa ya Oksijeni kwa wingi wakati sisi binadamu bado tunaendelea kuvuta hewa ileile ya Oksijeni.

"Kwa maana hiyo, nyakati usiku kunakuwa na upungufu wa hewa hiyo (Oksijeni) kwa sababu binadamu na mimea, wote tunatumia hewa moja."

Katika hali hiyo, Dk. Maduhu anasema ni rahisi sana kwa wagonjwa au watu wenye matatizo ya kupumua vizuri kufariki dunia nyakati hizo za usiku.

Anabainisha kuwa watu wanaoishi kwenye nyumba zilizo karibu na miti au majani ambayo yana hali ya kijani kibichi kwa nyakati au maua ya nyumbani, wana hatari kukabiliwa na upungufu wa Oksijeni kwenye maeneo yao.

"Hii ndiyo sababu kubwa kisayansi watu kufa usiku. Ni vizuri watu wakapanda miti hatua kadhaa mbali na nyumba zao hasa maeneo ya madirisha na kuepuka pia kupanda haya maua yenye majani yenye kijani kibichi na asili ya uteketeke kwenye madirisha au ndani ya sebule zao," anaonya.

Mtazamo huo wa Dk. Maduhu unaungwa mkono na Daktari Bingwa wa Usingizi na Mfumo wa Neva, Dk. Brandon Peters, ambaye katika chapisho lake la Mei 8 mwaka huu alilolipa jina la 'Why Do People Die in Their Sleep?' (Kwanini Watu Hufariki Dunia Usingizini?), anaanika sababu tisa za vifo vya usingizini.

Miongoni mwa visababishi vya vifo hivyo vilivyotajwa na Dk. Peters, ni shambulio la moyo kutokana na mwili kupokea kiwango kidogo cha Oksijeni wakati wa mtu akiwa usingizini pamoja na majanga (mfano tetemeko la ardhi), sumu mwilini na matumizi ya dawa za kulevya.

MAKALA

# Mambo ya kuzingatia lishe siku 1,000 ukuaji wa mtoto

Na Mary Geofrey



WATAALAMU wa masuala ya lishe wanatahadharisha kuwa mzazi akifanya makosa kwenye lishe ya mtoto katika siku 1,000 za mwanzo, basi mtoto husika anakuwa na udumavu wa akili, mwili au vyote viwili.

Mtafiti wa Mafunzo ya Lishe kutoka Taasisi ya Chakula na Lishe (TFNC), Victoria Kariathi, katika mahojiano na Nipashe, anabainisha kwa kina kuhusu dhana hiyo ya siku 1,000 za ukuaji wa mtoto.

Anasema siku 1,000 za ukuaji wa mtoto ndiyo msingi wa hatma ya afya ya ukuaji wa mtoto. Anasema siku hizo zinahesabiwa kuanzia siku ambayo mimba inatungwa hadi mtoto anapofikisha umri wa miaka miwili.

Kariathi anasema siku hizo pia zinagawanywa katika makundi ya kuanzia mimba inapotungwa hadi miezi tisa, sawa na siku 270, na kundi lingine linalojumlisha siku 730, sawa na miaka miwili ya kukua kwa mtoto tangu anapozaliwa.Anasema siku 1,000 ndiyo fursa ya uwekezaji wa ukuaji wa mtoto kwa maisha yake ya baadaye.

"Kama tukiwekeza katika siku hizi 1,000 za ukuaji wa kasi wa mtoto, tutakuwa tunafanya jambo muhimu sana la kumjengea maisha mazuri ya baadaye," anasema.

Kariathi anafafanua kuwa katika kipindi hicho, wazazi wakiwekeza vizuri, mtoto ataepuka maradhi ya udumavu wa akili na mwili.

**SIKU 270**

Katika kipindi hiki cha ujauzito, Kariathi anasema mama mjamzito anashauriwa kufika kituo cha afya kwa ajili ya kuanza kupewa ushauri wa masuala ya lishe na kinga za mama na mtoto mara tu anapogundua ana ujauzito.

"Ni muhimu mama apate ushauri kuhusu ulaji wake hasa ikizingatiwa kuwa wakati wa ujauzito kinachomsumbua mama mjamzito ni upungufu wa damu mwilini," anasema Kariathi.

Anabainisha kuwa mama mjamzito anapaswa kula vyakula mchanganyiko kulingana na makundi matano ya vyakula ambayo yanajumuisha vyakula vya nafaka, mizizi na ndizi.

Makundi mengine ni vyakula vya asili ya wanyama na jamii ya mikunde, mboga, matunda, mafuta, sukari na asali.

Kariathi anasema mama mjamzito pia anashauriwa kula vyakula vinavyoongeza damu kwa haraka ambavyo ni nyama za kila aina, maini na dagaa.

Anasema mama mjamzito pia anapaswa kujikita katika ulaji wa vyakula vya kundi la jamii ya mikunde vinavyoongeza damu ingawa siyo kwa wingi, hivyo anapaswa kula matunda pia.



**MIEZI 6 YA MTOTO**

Mtafiti huyo anabainisha kuwa, ni muhimu jamii kuzingatia kwamba mara tu baada ya mtoto kuzaliwa, kuanzia siku hiyo ya kwanza hadi mezi sita, hatakiwi kupewa chakula kingine chochote zaidi ya maziwa ya mama.

"Katika kipindi hiki mtoto asipewe kitu chochote isipokuwa dawa kwa ushauri wa daktari ili maziwa ya mama yaweze kumsaidia kumjenga kiafya na kiakili," anasema.

Kariathi anaendelea kufafanua kuwa maziwa ya mama yanamtosheleza mtoto katika kipindi chote cha miezi sita ya mwanzo kama mama atamnyonyesha vizuri.

Anasema jambo la kuzingatia ni kuhudhuria kliniki kwa ajili ya kupata ushauri wa namna ya kumnyonyesha mtoto maziwa kwa kuzingatia kumpa titi moja kwa muda mrefu ili apate maziwa mazito na mepesi. Anasema kama mama akipata tatizo wakati akinyonyesha, anapaswa kurudi katika kituo cha afya ili kupata ushauri wa wataalamu kwa ajili ya afya ya mtoto.

**MIEZI 6 HADI MIAKA MIWILI**

Mtafiti huyo anasema kuwa, katika kipindi cha kuanzia miezi sita hadi miaka miwili, mama anapaswa kumpa mtoto nyongeza ya vyakula.

Anasema vyakula anavyopaswa kupewa mtoto katika kipindi hicho, viende sambamba na unyonyeshaji wa maziwa ya mama.

Kariathi anasema mama anapaswa kumwandalia mtoto vyakula vilivyo katika makundi matano ya vyakula na vilivyopondwa au kusagwa. Anasema chakula anachopaswa kula mtoto ni kizito, kilaini na kilichoandaliwa katika utaratibu mzuri. Anasema kuwa wakati huo mtoto anapaswa kupewa pia maji ya kunywa na matunda ili kupata virutubisho vinavyotakiwa kwenye mwili.

"Mama hapaswi kumpa mtoto mchuzi wa mboga, samaki au nyama, bali anapaswa kumsagia vyakula hivyo ili kupata virutubisho vinavyotakiwa," anasisitiza Kariathi.

**MADHARA YA UZEMBE**

Mtaalam huyo wa lishe anasema watoto wakikosa lishe katika siku hizo 1,000 wanapata athari kubwa zitokanazo na lishe duni.

Anasema lishe duni husababisha mtoto kuwa na uzito pungufu kulingana na umri wake au kuwa na ukondefu unaojitokeza kama mtoto hatapata chakula kama inavyotakiwa au magonjwa.

Anasema mtoto akipata uzito pungufu, yupo kwenye hatari ya kupata udumavu ambao huanza taratibu na kuja kujitokeza siku za baadaye kama kushindwa kurefuka. Kariathi anasema, athari za udumavu unaosababishwa na lishe duni katika siku 1,000 haziwezi kurekebishika baada ya kipindi cha miaka miwili kupita.

Anaongeza kuwa, kama mama hakuzingatia lishe inayofaa, kuna uwezekano mkubwa kuzaa mtoto mwenye uzito upungufu unaosababisha kupata magonjwa mengine.

**NINI KIFANYIKE?**

Kariathi anasema jamii izingatie elimu inayotolewa na watoa huduma za afya na kuondokana na dhana potofu zinazoweza kusababisha madhara kama hayo.

"Mila potofu za kuanza kuwalisha watoto vyakula kabla ya kufikisha miezi sita zinasababisha madhara makubwa kama viribatumbo na udumavu. Pia, wazazi wanapaswa kuzingatia ushauri wa wataalamu katika kipindi chote cha malezi," anasema.

Anasema kila zahanati nchini imeagizwa kuwa na utaratibu wa kutoa elimu kwa mama mjamzito hadi mama kujifungua na namna ya kumlea mtoto hadi kufikisha miaka minne, hivyo jamii inapaswa kufuata ushauri unaotolewa.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Jamii ijenge utamaduni wa kupima afya kuzuia kuenea maradhi na vifo*

**UGONJWA** wa saratani umeendelea kuwa tishio kwa maelfu ya watu nchini na mamilioni kwa Afrika na dunia kwa ujumla huku sababu mbalimbali zikitajwa kuwa ni chanzo cha tatizo hilo.

Kutokana na ugonjwa huo kugharimu maisha ya watu huku wengi wakifariki dunia, wengine kuendelea kuteseka na baadhi kukosa viungo vya miili kutokana na kukatwa ili kuzuia kusambaa zaidi mwilini, zimeibuka taarifa mpya kuhusu visababishi ambavyo vinachochea tatizo hilo kuwa kubwa zaidi.

Taarifa hizo zilizotolewa na Taasisi ya Saratani ya Ocean Road (ORCI) zinabainisha kuwa mfumo wa maisha hasa kwa watu wanaoishi kwenye miji mikubwa, unachangia ugonjwa huo kuendelea kuwa tishio na kugharimu maisha ya watu.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Huduma za Kinga wa ORCI, ukubwa wa tatizo la saratani unazidi kuongezeka huku akibainisha kuwa Tanzania kwa sasa inakadiriwa kuwa na zaidi ya watu 42,000 wanaosumbuliwa na maradhi hayo.

Idadi hiyo ni ongezeko kubwa kulinganisha na takwimu za mwaka 2010 zinazoonyesha kuwa katika kipindi hicho, watu waliofika na kupatiwa tiba kwa haraka walikuwa 2,800 tu.

Ongezeko hilo, kwa mujibu wa mtaalamu huyo, linaonekana kusababishwa na kuwapo kwa aina mpya za saratani tofauti na zile zilizozoeleka kama vile utumbo, mlango wa kizazi na shingo ya kizazi. Lakini sasa kuibuka kwa tatizo la tezi dume kumechangia ongezeko la saratani miongoni mwa watu duniani, Tanzania ikiwamo.

Aina hyo ya saratani, mtaalamu huyo anabainisha kwamba imesababisha madhara na kugharimu hata maisha ya vijana wenye umri wa miaka 30 tofauti na zamani ilivyokuwa ikijulikana kwamba wanaokumbwa hata kufa kwa maradhi hayo ni watu wazima hususan wenye zaidi ya miaka 60.

Pamoja na kuibuka kwa aina mpya na kuongeza ukubwa wa tatizo, chanzo kingine, pengine kikubwa ni watu kutokuwa na tabia ya kufanyiwa uchunguzi wa afya mara kwa mara.

Kwa ujumla, utamaduni huo kwa wengi umekuwa msamiati mgumu. Watalaamu wanabainisha kuwa visababishi vya saratani huanza kujitokeza mapema lakini mpaka kujulikana ni baada ya miaka 15 hadi 20.

Hali hiyo inaonyesha kuwa kama watu watajenga utamaduni wa kufanyiwa uchunguzi wa afya mara kwa mara, saratani na maradhi mengine yanaweza kudhibitiwa na hata kuwezesha watu wengi kuepukana na vifo tofauti na ilivyo sasa.


Kutokana na ukweli huo, ni vyema sasa hatua za makusudi zikachukuliwa kuhamasisha watu kujenga tabia ya kufanyiwa uchunguzi wa afya mara kwa mara ili pale inapobainika kuna viashiria vya saratasni au ugonjwa wowote, matibabu yakafanywa mapema ili kuokoa maelfu ya watu kupoteza maisha.

Ni ukweli kwamba watu wengi wamekuwa wakifika katika vituo vya huduma za afya ugonjwa ukiwa umeshafikia hatua ya juu, jambo ambalo linakuwa gumu kupatiwa matibabu stahiki.

Ni imani yetu kwamba kama uchunguzi wa maradhi mbalimbali utafanyika, nchi itakuwa na hazina kubwa ya nguvu kazi ambayo itakuwa kichocheo kikubwa katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Kila mtu katika nafasi yake, anapaswa kuwa balozi wa kuhamasisha utamaduni wa kupima afya ili kuwahi matibabu kabla ugonjwa haujafikia hatua mbaya.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# *Utendaji kazi wa taasisi hizi kero serikali awamu ya tano*

Na Mwandishi Wetu

**SERIKALI** ya awamu ya tano, katika moja ya mambo ambayo imekuwa ikisisitiza ni utendaji kazi wenye kujali matakwa ya wananchi na kutoa huduma za viwango vya juu na zenye tija.

Katika kuhakikisha hilo linafanikiwa, serikali imekuwa ikiziagiza taasisi zilizo chini yake kuwahudumia wateja kwa kasi na kwa weledi wa hali ya juu.

Miongoni mwa taasisi zinazotoa huduma ni pamoja na mamlaka za serikali za mitaa kwa maana ya halmashauri kupitia idara mbalimbali mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira, Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF).

Licha ya kwamba msisitizo umekuwa mkubwa katika serikali ya awamu hii na hata kuchukua hatua dhidi ya watu wanaoshindwa kutekeleza wajibu wao, jambo hilo ni la muda mrefu tangu serikali ya awamu ya kwanza chini ya Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere.

Itakumbukwa kuwa mwaka 2002 wizara za serikali pamoja na idara zinazojitegemea na mashirika ya umeme ilianzisha rasmi mkataba wa huduma kwa mteja katika tendo la kihistoria lililofanyika mjini Dodoma. Mgeni rasmi katika uzinduzi huo alikuwa Spika wa Bunge kwa wakati huo, Pius Msekwa.

Pamoja na miongozo, mikataba ya huduma kwa wateja katika taasisi mbalimbali kuwapo, utendaji kazi na utoaji wa huduma katika baadhi ya taasisi za serikali ni wa kusikitisha. Kwa maneno mengine ni wa mwendo wa kusuasua.

Moja ya taasisi ambazo zimekuwa zikilalamikiwa ni NIDA ambayo utoaji wa vitambulisho wa taifa umekuwa na walakini kutokana na maombi kuchukua muda mrefu. Ukienda hivi sasa katika ofisi za mamlaka hiyo, utakuta watu wamejazana wakifuatilia huduma hizo bila mafanikio.

> **Moja ya taasisi ambazo zimekuwa zikilalamikiwa ni NIDA ambayo utoaji wa vitambulisho wa taifa umekuwa na walakini kutokana na maombi kuchukua muda mrefu. Ukienda hivi sasa katika ofisi za mamlaka hiyo, utakuta watu wamejazana wakifuatilia huduma hizo bila mafanikio.**

Katika ofisi moja jijini Dar es Salaam, siku moja baadhi ya watu walikuwa wakilalamika kuwa pamoja na kuambiwa tangu mwaka jana kuwa uchakataji (msamiati ulioibua urasimu na umangimeza katika utendaji kazi) unaendelea lakini hadi sasa imekuwa hadithi ya alfu ulela ulela.

Hakuna dalili zozote za upatikanaji wa vitambulisho pamoja na kwamba watendaji wanajisifu kuwa wameshatoa namba ambazo zinaweza kutumika kupata huduma mbalimbali kwenye taasisi za serikali hususan zile zinazohitaji kuwa na namba ya NIDA.

Taasisi nyingine ambayo nayo imekuwa na mazonge ni NHIF ambayo mtu akitaka kupata kadi kwa ajili ya matibabu baada ya kulipia ni lazima asubiri miezi mitatu! Ukiuliza unajibiwa kuwa mchakato unachukua muda huo na moja kwa moja watakuonyesha kipengele cha muda kwenye fomu ya maombi.

Jambo la kujiuliza ni kwa nini mchakato wa kupata kadi kutoka kwenye taasisi hizo kuchukua siku 90 hadi zaidi ya miezi 12? Kama mashine zipo tatizo linatokana na nini?

Kila mtu anafahamu kuwa katika zama hizi za maendeleo ya sayansi na teknolojia, suala la kutengeneza kadi linaweza kuchukua muda mfupi kama ilivyo kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) ambayo inamchukua mtu muda mfupi tangu kujiandikisha hadi kupata kadi.

Ni vyema taasisi hizi na zingine zenye mtindo wa umangimeza na urasimu wa muda mrefu, uliopambwa na utetezi usio na mashiko, zikabadilika na kufanya mambo kidigitali badala ya kuendelea kufanya kama enzi za matumizi ya mikono.

SAFU

## FIKRA MBADALA



Nkwazi Mhango, Canada

# Nini kosa JPM kujenga uwanja wa ndege, mbuga Chato?

KITENDO cha serikali kujenga uwanja wa ndege mkoani Geita kimewakera baadhi. Mgombea fulani alisikika akilalamikia kuanzishwa mbuga ya wanyama mkoani Geita kiasi cha kuigeuza sera. Jamani, kama hamna cha kumpinga Rais John Magufuli heri mjinyamazie kuliko kujiaibisha.

Jamaa anasema hii ni aibu na Watanzania si wajinga. Kweli. Watanzania si wajinga. Ulizeni vigezo vilivyotumika kujenga uwanja husika. Je huyu hajui kuwa dhahabu inayopatikana sana Geita ni ya pili kwa kuchangia pato la taifa? Je, hajui kuwa wachimbaji wengi wa dhahabu huko licha ya kampuni kubwa kuliko zote ya GGM wako Geita? Je, hajui kuwa wachimbaji wengi ni matajiri wanaotaka usafiri haraka? Je, kama mkoa wenye kuzalisha dhahabu nyingi; hivi kosa ni kuwa na uwanja wa ndege wa kimataifa?

Chato ni 'tactical' kiusalama na 'alternative' kwa ndege zinapokuwa na dharura nchini na majirani. Geita ina vivutio vinavyohitaji usafiri wa haraka.

Alitaka aanzishe uwanja wa mpira? Umuhimu wa Chato kwa dharura ni sawa na ule wa Anchorage Alaska kwa ndege za kimataifa. Walalamikaji hawajui: Chato-Burigi ni ya tatu kwa ukubwa baada ya Ruaha na Serengeti. Je, walitaka hii mbuga iendelee kutumika kifisadi kama zilivyokuwa nyingine alizoanzisha hivi karibuni au makazi ya majangili na majambazi? Je, hawajui kuanzisha mbuga, zaidi ya kuongeza mapato kimkoa na nchi, huzalisha ajira mbali na usalama wa wanyama, mazingira na nchi kwa ujumla? Je, kosa la Magufuli ni kuzaliwa kwenye sehemu yenye Wanyama? Mbona wahusika hawalalamikii mbuga nyingine zilizoanzishwa sambamba na mbuga hii wala viwanja vya ndege vilivyojengwa sambamba na hiki kinachomnyima usingizi?

Kwanini wahusika wasifanye japo 'homework' kidogo wajiulize: Kwanini Geita inayoingiza mabilioni ya shilingi kiuchumi kitaifa isiwe na uwanja wa ndege, lakini Zanzibar ambayo pato inaloiingiza haliwezi kulingana na Geita iwe na uwanja wa ndege wa kimataifa? Kwanini hawalalamikii Mbeya kuwa na uwanja wa kimataifa wa ndege wala Mwanza?

Hata angepanua uwanja wa ndege wa Mwanza na kuacha kujenga wa Chato bado wangesema anapendelea Kanda ya Ziwa. Haya ndiyo mawazo ya watu wanaoshindwa kufikiri sawa sawa na kuhukumu mambo kama yalivyo baada ya kufanya hivyo kwa kusukumwa na hasira na kutaka umaarufu rahisi na kulipiza kisasi. Wanaobeza juhudi za Magufuli wanapaswa kuwa na busara japo kidogo.

Niliwahi kusikia profesa mmoja mstaafu aking'aka eti watu wanasifia barabara, madaraja, ndege na reli. Anataka wasifie umaskini uliofanya kuzidiwa na viinchi visivyo na rasilimali? Profesa huyu alisikika akimnukuu na akitaka kumtumia Marehemu Baba wa Taifa Mwl. Julius Nyerere aliyesema kuwa maendeleo lazima yawe ya watu. Ama! Kwani hii miundombinu imejengwa isafirishe wanyama au majini? Hawa wanaopiga kelele watakuwa wa kwanza kuvitumia.

Wahenga wanaasa: Mnyonge mnyongeni: haki yake mpeni. Wapo waliosema kuwa hata makaburu walijenga miundombinu. Ni kweli. Kwanini hawajiulizi: makaburu walimjengea nani kama siyo weupe tu wakifaidi vitu hivyo kwa jasho la Mswahili? Ajabu hao wanaomzodoa na kumlaani Magufuli kwa kujenga vitu 'badala ya utu' ni hao hao walioukuwa wakisafiri toka kwao kupitia Uganda na Kenya kwenda Dar es Salaam.

Tumekuwa wepesi wa kusahau hivi kwa malengo ya kisiasa kiasi cha kujigeuza kwa makusudi wezi wa fadhila? Walitaka Magufuli ajenge nini zaidi ya miundombinu ili kufanya mageuzi ya uchumi wa kisasa? Hao wakienda Ulaya wakapanda vipandwa wanavyolalamikia; wakija huku wanasema kwanini hatuwi kama Ulaya? Tukitaka kuwa kama Ulaya wanayoiabudia, wanaanza nongwa. Hii ni tabia ya kitoto. Mtoto ukimpa mpira achezee akaupoteza anakulaumu. Ukimnyima ili asiupoteze anakulaumu.

Kimsingi, wanaompinga Magufuli watafute na kujenga hoja zenye mashiko badala ya uzushi na siasa za maji taka. Tuache siasa chafu. Watanzania si wajinga wala wasahaulifu hivyo wala si vipofu na viziwi.

Serikali iko mbioni kujenga hospitali za rufaa mikoani. Kesho utasikia Magufuli kajenga hospitali ya rufaa kwao. Je, kwao hawaugui; si Watanzania sawa na wengine wanaohitaji huduma hii; kumzaa Magufuli inapoteza haki zinazopewa mikoa mingine? Ni ajabu kusikia wakisema eti Geita hakuna biashara ya kuhitaji ndege.

Mbona Arusha na Kilimanjaro kuna uwanja wa ndege wa kimataifa? Wazidi kutukana kuwa uwanja wa ndege wa Chato hauna kazi bali kutumika kumsafirisha Magufuli na mama yake. Haya matusi ya nguoni yasiyopaswa kuvumiliwa. Pia si maneno ya kistaarabu. Nadhani tujadili hoja badala ya familia za wagombea kwani, wanafamilia si wagombea. Pia wanadai eti Nyerere hakujenga uwanja wa ndege kwao.

Angejengaje wakati ule vipaumbele vilikuwa ni siasa za ukombozi Kusini mwa Afrika?

Angejengaje wakati hata barabara zenyewe hazikuwa zimejengwa kutokana na jukumu la Tanzania kumpiga nduli Idi Amin? Hakika, hata Nyerere angekuwa hai leo, angemwambia Magufuli akachape kazi kama ambavyo mzee Ali Hassan Mwinyi, Marehemu Benjamin Mkapa na Jakaya Kikwete walichagiza; si mara moja wala mbili.

Kumalizia, kuwasaidia wenzetu kufikiri kuwa kinachoendelea, si kwa faida ya Tanzania tu bali hata majirani zetu hasa nchi zisizokuwa na bandari kama vile Rwanda, Uganda, Zambia, Malawi na DRC. Muhimu, kukubali na kuelewa: ndege zitazidi kununuliwa, barabara na madaraja kujengwa na mbuga mpya za wanyama kuanzishwa kwa faida ya Watanzania watake wasitake.

Binadamu tuna tatizo moja kubwa kimajaaliwa: kusahau tena kwa wengine haraka na kirahisi. Mpeni muda arekebishe Tanzania basi.

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO



Na Joseph Kulangwa

# Jamani watoto wa kambooo!

TUKIWA wadogo, bado tunaishi mashambani, tulikuwa ndugu, tukishirikiana kwa mambo mbalimbali bila hata kujua haraka huyu ni mtoto wa nani na hasa katika familia za mitala. Familia ambazo kulikuwa na mume mmoja wake wengi, lakini tukiishi mji mmoja.

Sote tuliitana ndugu na kuheshimiana kwa kuzingatia umri na jinsi. Ndiyo kama ulivyokuwa mfumo dume, watoto wa kiume tuliheshimiwa na kunyenyekewa na wale wa kike. Amini usiamini, dada mkubwa alimpigia magoti mdogo wake wa kiume. Mfumo uliruhusu.

Enzi hizo hatukupata kusikia kuwapo kwa baba, mama au mtoto wa kambo! Na hata kama neno hilo lilitamkwa, hakuna aliyejua maana yake haraka.

Pengine lilikuwa la kigeni na ndiyo sababu hatukusumbuka kulifuatilia, ingawa tulikujaambiwa kuwa baba, mama au mtoto wa kambo si wa kuzaliwa katika muunganiko wa familia husika.

Yaani kumbe alikuwa mtu wa kufikia tu katika familia, hakuwa ndugu wa damu. Na kama walikuwapo hao haikuwa rahisi kutambua kuwa huyu ni wa damu au huyu ni wa kambo, kwa sababu tulishirikiana na kupendana na kuheshimiana katika kila kitu.

Maisha yalipozidi kusonga mbele, ndipo sasa tukaja kuona pengo hilo. Uchumi ulipoanza kuwaingia watu katika jamii, tukaanza kubaguana kuwa huyu wa damu na huyu la hasha. Tukaanza kusikia aah yule si baba yake ni baba wa kambo, yule si mama yake ni mama wa kambo, huyu si mwanawe ni mtoto wake wa kambo. Nakadhalika.

Pengo hilo au ufa huo, ukaibua chuki, si tu baina ya wazazi na watoto, lakini mpaka watoto wenyewe wakaanza kubaguana na kutambiana, wewe ni wa kambo huna haki hapa. Hakika watoto wa kambo wakaanza kubaguliwa, wakaanza kunyanyaswa, wakasingiziwa kila baya lililotokea.

Kila kilichopotea nyumbani kwenye familia, mtoto wa kambo akawa mtuhumiwa namba moja, kila kilichoharibika mtoto wa kambo aliulizwa kwanza. Hivyo wale wa damu nao wakaona wawatumie wale wa kambo kama kichaka. Kila wakiharibu walikimbilia kwa wazazi kuwashitaki wenzao wa kambo.

Nao wa kambo wakajiona kunyanyapaliwa, wakajitahidi kuwa waangalifu na kujiepusha hata kukaa karibu na vyombo vinavyovunjika, kwamba isijetokea bilauri ya udongo ikadondoka na kupasuka akasingiziwa hata kama ilisukumwa na mbwa.

Wakajiona hawana nafasi tena katika familia husika, wengine wenye roho ngumu wakajiondoa akili na kuamua kuwa na tabia mbaya za wazi tu, baada ya kuona kusingiziwa kumekithiri. Wakajiapisha liwalo na liwe, kwa sababu hata wakifanya lililo jema walionekana waovu, kwa kuwa tu ni watoto wa kambo.

Ikawa sasa kila zuri likifanyika katika familia, watoto wa damu walipewa sifa, na hata kama lilifanywa na mtoto wa kambo, aliambiwa bila mtoto wa damu kusaidia lisingefanyika. Ili mradi watoto wa kambo wakaonekana hawafai katika jamii, hawana jema katika jamii, hawana mchango chanya katika jamii.

Walipopelekwa shule, aliyenunuliwa sare kwanza ni mtoto wa damu, wale wa kambo walisubiri msimu ujao wa pamba. Vinginevyo wavae masulupwete yaliyoachwa na wale wa damu. Na wakati mwingine madaftari yenye mwandiko mzuri hata kama ni ya mtoto wa kambo, yalilazimika kusingiziwa kuwa ni ya watoto wa damu.

Mtoto wa damu aliyeonekana nunda au kilaza, hakuzomewa kama wale wa kambo, bali alitiwa moyo na kuambiwa ni utoto tu, akikua atapata tu akili, lakini wa kambo aliambiwa amerithi akili za wazazi wake huko alikozaliwa. Wa damu ndiye ajuaye kila kitu, ndiye ajuaye kusoma na kuandika, ndiye ajuaye kuchora na kuchonga.

Hivi nani alisema mtoto wa kambo ndiye asiyejua kila kitu na ndiye asiyefaa katika jamii? Nani alisema? Aaah jamani, hivi kweli tunataka kuaminishwa hivyo? Mnayaona msijifanye hamwoni kinachofanyika leo katika nchi hii!

Hamkuona mapingamizi? Hawajui kuandika majina yao, hawajui kuandika majina ya vyama vyao, kweli? Wa kambo tu ndio hawajui hayo, lakini wale wa damu? Acheni kamchezo hako bhana. Tu sawa mbele ya Maulana ambaye anatuona!

## KONA YA UKWELI



Na Thobias Mwanakatwe

# Ziko wapi ilani za vyama vya siasa kwenye uchaguzi huu?

KAMPENI za Uchaguzi Mkuu kwa ajili ya rais, wabunge na madiwani unaotarajia kufanyika Oktoba 28, mwaka huu zilianza rasmi Agosti 26 baada ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kufanya uteuzi wa wagombea wa vyama mbalimbali vya siasa.

Hata hivyo, kitu kimoja ambacho kimenisukuma kuandika makala hii ni kasoro moja kubwa kuhusu suala zima la vyama vingi kutolipa umuhimu suala la ilani za uchaguzi.

Ilani ni suala muhimu sana katika uchaguzi wowote wa kidemokrasia. Ni kitu kikubwa na cha msingi ambacho kinapaswa kuwekwa wazi na vyama vya siasa kabla ya kuingia kwenye kampeni.

Ilani haina budi kuelezwa kwa umma mapema kabla ya uchaguzi kwani ndiyo inayotarajiwa kunadiwa na kila chama cha siasa kwa wapigakura ili wafanye uchambuzi wa kina na hatimaye kukichagua kuongoza dola.

Andiko hilo linalojumuisha masuala mbalimbali yakiwamo ya kijamii na kiuchumi, ndilo linaloeleza mambo muhimu ambayo chama husika kitayatekeleza kwa kipindi fulani ikiwa kitapewa ridhaa ya kushika hatamu za uongozi.

Hapa nchini kuna tabia iliyojengeka miongoni mwa baadhi ya vyama vya siasa kuchelewa kutangaza ilani zao hadi hatua za mwisho na vingine kwenda nje ya ilani zao kwa kuhubiri vurugu na maandamano kwenye majukwaa ya kampeni.

Vyama vya siasa vinapaswa kutambua kuwa wapiga kura wanatakiwa kutangaziwa ilani za vyama za siasa ili waweze kizisoma na kuzielewa pamoja na kuzifanyia uchambuzi wa kina kabla ya kampeni za uchaguzi kuanza.

Katika uchaguzi wa mwaka huu, takriban vyama 15 vimesimamisha wagombea kwenye udiwani, ubunge na urais lakini cha kushangaza ni vyama visivyozidi vitano ambavyo vimeweka wazi kuhusu ilani zao.

Jambo lingine ambalo limeshushudiwa katika kipindi hiki ni baadhi ya vyama vilivyozindua kampeni zao wagombea wao wanapozungumza mambo ambayo yapo nje ya ilani zao, hakika huku ni kuwachezea Watanzania.

Pamoja na kwamba vyama vinachelewa kuweka wazi ilani zao pengine kwa visingizio vya maandalizi yanayohitaji utaalam, ukweli unabaki pale pale kuwa hivi sasa ilani za vyama vya siasa zinapaswa kulenga mambo muhimu yanayowakumba wananchi kwenye maeneo yao.

Ilani zinapaswa kulenga changamoto hasa za afya, elimu, mazingira, miundombinu, kilimo nakadharika. Hizi ndizo ajenda muhimu kwa duniani hivi sasa. Mambo mengine kwa sasa hayana nafasi kubwa.

Kwa maana hiyo, ilani za uchaguzi za vyama vya siasa hazina budi kutoa kipaumbele kwa maswala hayo ili kulenga matatizo halisi na ya msingi yanayoikumba jamii kwa ujumla.

Unapozungumzia umaskini unalenga mambo yote ya msingi yanayowakabili Watanzania wengi ambayo ndani yake kuna umaskini, elimu, ukosefu wa ajira na kadhalika.

Katika kampeni hizi Watanzania hawapendi kusikia matusi na malumbano ya kisiasa kutoka kwenye majukwaa ya kampeni bali kuona na kusikia vyama vinanadi ilani zao ambazo zinaeleza mikakati na mbinu za kuwaletea maendeleo Watanzania.

Katika kipindi hiki, Watanzania tusikubali kuchagua viongozi ambao hawana ilani za vyama vyao na wale ambao wanahubiri vurugu kwani amani ya nchi yenu ni tunu tusiichezee.

Tukichagua vyama visivyokuwa na ilani wala Sera tutakuwa tunajitumbukiza kwenye matatizo na tutaumia kwa kipindi cha miaka mitano.

**MUNGU IBARIKI TANZANIA**

**mwanakatwe2015@gmail.com**

## DARASA LA NDOA



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka
0655865555

# Nafasi ya fedha katika uhusiano wa wanandoa

FEDHA ni njema na mtu kuwa nayo si uovu wala dhambi. Nafasi anayoipa mtu katika maisha yake ndiyo itakayoamua kama ni njema au mbaya. Ni njema ikitafutwa kwa halali na kutumika vizuri kwani inaweza kuwa nyenzo ya kuleta maendeleo.

Hata hivyo, fedha ina uwezo wa kuleta maumivu na kugeuka kuwa shina la ubaya isipotumika vizuri. Fedha ina nguvu katika maisha ya mtu binafsi na katika uhusiano na watu wengine.

Ziko baadhi ya ndoa zilizoimarika baada ya kupata fedha na wanandoa kufurahia mafanikio. Lakini zipo ndoa zilizoharibika baada ya fedha kuingia. Fedha ipo lakini ndoa haipo. Baadhi ya wanandoa hawafurahii maisha ya ndoa pamoja kwamba wanazo fedha. Fedha imegeuka kuwa kama kirusi cha corona, hivyo kuharibu ndoa na uhusiano wa wanandoa.

Utafiti mbalimbali unaonyesha kuwa migogoro mingi ya wanandoa hutokana na mambo yanayohusu fedha. Matumizi ya fedha yamesababisha matatizo mengi katika ndoa nyingi. Ubinafsi umezielemea ndoa nyingi. Tatizo linakuwa kubwa hasa pale fedha ya mume inapoonekana haimhusu mke, hivyo mke kutotakiwa kuhoji au kuchangia mawazo yoyote juu ya matumizi ya fedha. Kadhalika, wapo wanawake ambao hufanya vivyo hivyo dhidi ya waume zao.

Mfumo dume katika jamii umeongeza ukubwa wa tatizo hili. Suala la fedha ameachiwa mume bila mke kuwajibika, kujua au kuchangia lolote. Wanawake wenyewe wengi wao wamewaachia waume kuwajibika kwa kila kitu kinachohusu fedha na katika uamuzi unaohusu fedha ndani ya ndoa.

Pia kuna uamuzi mwingine umeangamiza familia kwa sababu ni mtu mmoja. Mume au baba tu katika ndoa ndio hutoa uamuzi kuhusu mambo yanayohusu fedha.

Katika zama hizi ulimwengu umebadilika. Wanawake wengi nao wana uwezo wa kifedha kwani wanafanya kazi, biashara na kuingiza pato katika familia na ndoa.

Uzoefu unaonyesha kuwa, ziko familia nyingine ambazo mke ndiye mwenye kipato kikubwa kuliko mume. Hali hii imesababisha baadhi ya waume kujisikia duni kwa wake zao na kupoteza hali yao ya kujiamini.

Fedha huleta mihemko. Baadhi ya wanandoa ambao walikuwa wema, wastaarabu na watulivu fedha ilipokuwa haipo, ilipopatikana na mafanikio ya kiuchumi kuwapo, mafanikio hayo yakageuka kuwa chanzo cha matatizo katika ndoa. Fedha imeondoa utulivu uliozoeleka na kubomoa ndoa.

Baadhi ya waume wakipata fedha, ndio mwanzo wa ukatili katika familia na unyanyasaji kwa wake zao. Uhusiano mpya huanzishwa nje ya ndoa (michepuko) na fedha hupata matumizi makubwa zaidi, hivyo kudumaza ustawi wa ndoa na familia.

Wako pia baadhi ya wanawake ambao wakifanikiwa na kuwa na kipato kikubwa kuliko mume, kiburi na dharau huinuka dhidi ya mume. Mahali pengine, mume huishi kama kibarua ndani ya nyumba yake.

Kauli mbaya za mke kwa mumewe huwa jambo la kawaida. Mke hutumia fedha anavyotaka na kufanya mambo anavyojisikia bila kumshirikisha na kukubaliana na mumewe.

Heshima kwa mume hupungua kama si kuondoka kabisa. Mbaya zaidi, baadhi ya wanawake husahau kutimiza majukumu yao ya kindoa kwa waume zao. Mazingira kama haya yanafanya mustakabali wa ndoa kuwa shakani.

Wanandoa waliishi kwa amani kabla ya kufanikiwa kiuchumi na kimaisha. Lakini baada ya kupata mafanikio, wanandoa wamebadilika na kuanza kuumizana. Thamani ya mwenzi imepotea. Mwenzi anaonekana ni mtu asiyeendana na hadhi ya mwenzake.

Fedha imependwa zaidi kuliko mwenzi au familia. Hali hii imesababisha kwa sehemu kubwa baadhi ya wanandoa kutengana na ndoa kuvunjika. Athari zake ni kubwa si kwa wanandoa wenyewe tu, bali kwa watoto ambao huathirika kiroho, kisaikolojia, na kimakuzi. Watoto wanakosa malezi bora, furaha na kujisikia kutokuwa salama re) kwa sababu ya kukosekana uwapo wa baba au mama.

Mafanikio ya kiuchumi ya mtu yeyote yanahitaji mipango na nidhamu katika fedha. Watu wengi hushindwa kufikia malengo na kufurahia maisha kwa sababu ya kukosa mipango na nidhamu katika fedha.

Kupanga na kuwa na nidhamu katika matumizi ya fedha ni busara na hekima. Mpango huanzia kwenye kipato kidogo, si lazima kuwa na kipato kikubwa.

Kwa hiyo, wanandoa wakitaka kufanikiwa kiuchumi wajifunze kupanga pamoja hata kama kipato ni kidogo.

Tabia nzuri ya kuijenga na kuiendeleza tangu mwanzo wa ndoa ni ile ya kujipangia bajeti ya familia. Hii husaidia kuelewa ni fedha kiasi gani zinapatikana na kupanga jinsi gani zitatumika.

Ni jambo la kawaida kimahesabu kwamba, matumizi ya fedha yasizidi uwezo wa kimapato. Wanandoa waishi kulingana na kipato chao, huku wakijilinda dhidi ya mashinikizo na tamaa.

Wanandoa pia wajifunze kuishi maisha yao na si ya wengine. Wanachokipata wakitumie kwa nidhamu kwa ajili ya maendeleo ya familia, huku wakimshukuru Mungu na kuridhika.

■ **Dk. Mlyuka ni Mchungaji wa KKKT, mtafiti mshauri na mwanataaluma. Pia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care (MaMCare) inayojihusisha na masuala ya ndoa na malezi. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa: enomlyuka@gmail.com**

MAISHA
SEPTEMBA 13, 2020
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
Jumapili



HARUSI

Ukurasa 12



Mwelekeze mwanao kabla hajapotezwa

Ukurasa 10



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Samani huongeza mvuto wa nyumba



Smoothie ya strawberries na ndizi

Ukurasa 14



# CHEKO MURUA: Raha uwe na meno meupe

Ukurasa 14

# Mwelekeze mwanao kabla hajapotezwa

KWA wazazi wengi 'wenye adabu zao', pengine jambo hili linaweza kuonekana kama kukiuka maadili na upotevu usiokubalika kijamii, eti mzazi akae na mwanawe wa miaka 16 hadi 20 na wazungumzie misukosuko ya kimapenzi inayomkabili.

Kukosa adabu zaidi, katika hili, mtoto mwenyewe anayetakiwa akae naye na kuzungumzia masuala ya mapenzi ndio kwanza anasoma pengine kidato cha tatu au ndio kwanza amemaliza 'form six'!

**Iko hivi:**

Mwanao wa umri huo, ambaye unaamini kuwa bado mdogo, anaonekana hana furaha na kila mara amezongwa na mawazo kiasi kwamba hata kula kwake kumekuwa kwa kujilazimisha na kila anapokaa anaonekana mnyonge mno.

Umejaribu kumuuliza, wewe mwenyewe, na pengina ukatumia hata rafiki zake wakueleze anatatizwa na nini, lakini hujapata jibu sahihi, yeye mwenyewe anakujibu; "Hamna kitu (baba au mama)" na wenzake nao wanakuambia; "Hata hatujui anasumbuliwa na nini".

Nyuma ya maswali yako na mbele ya ukimya wake kuna jambo moja linalosababisha hali hiyo aliyonayo mtoto wako, awe mvulana au msichana, na jambo lenyewe ni msukosuko wa kwanza wa mapenzi aliokutana nao katika safari ndefu ya mapenzi aliyoianza.

Kilichosababisha hali hiyo, inayowakuta matineja wengi, ni kwamba ana mpenzi wake ambaye kwa akili zao za kitoto waliamini kuwa walipendana kwa sababu za kuvutiwa na maumbo yao, kila mmoja amezama kwa mwenzake.

Wakiwa kwenye uhusiano huo, uliosababisha furaha kubwa baina yao, inatokea mtu mzima mmoja au kijana mwingine mwenye uwezo kuliko mtoto wako anaingilia penzi lao na kuwatenganisha kwa zawadi na fedha anazompenzi wa mwanao naye anaamua kuachana na mwanao. Hili ndilo linalomletea tafarani yote hiyo.

Tangu akiwa mdogo ulishamuonyesha kuwa katika kila hali mapenzi au kuwa na 'mchumba' ni jambo linalofanywa na watoto 'wa kishenzi' na katika umri wake wote huo amezingatia hilo na kuamini kuwa ikitokea siku ukafahamu kuwa ana 'mchumba', basi lazima 'atakiona cha mtema kuni'!

Moja ya madhara makubwa yanayoonekana kuwakera wazazi wengi, ingawa baadaye hugeuka kuwa ni mzigo wanaoubeba wenyewe, ni lile la kuwapo kwa mimba nyingi za utotoni kwa wazazi wenye watoto wa kike ambao huingia kwenye vishawishi vya mapenzi bila ya kujua athari za baadaye juu ya jambo hilo.

Ingawa wazazi wengi huonyesha hasira na kufikia hata kuwatimua watoto hao majumbani mwao, lakini uzoefu unaonyesha muda mfupi baada ya watoto kujifungua na 'mjukuu' kuonekana wazazi wale wale waliokuwa wakali hapo awali hurudisha mioyo yao na kuwapokea mabinti na wajukuu zao ambao wengi huwa wametelekezwa na baba wa watoto zao.

Ukiachilia mbali ujauzito wa utotoni, lipo pia suala la maambukizi ya virusi vya UKIMWI kwa watoto wa jinsia zote ambalo nalo lingeweza kuzuilika iwapo kama wazazi wengekuwa 'marafiki' kwa watoto wao na kuwapa muongozo sahihi wa kukabiliana na masuala ya mapenzi katika umri mdogo.

Tafiti nyingi zilizofanywa katika Bara la Afrika na Asia zinaonyesha kuwepo na 'ukakasi' wa wazazi kuzungumza masuala ya mapenzi na watoto wao. Kwa hali hiyo watafiti wamekuwa wakitoa ushauri kwa wazazi wenye kukabiliwa na hali hiyo kuwatafutia watoto wao watu wazima wengine ili wazungumze na watoto wao.

Katika hili inashauriwa kuwa wazazi wawe makini katika kuteua mtu wa kuzungumza na watoto wao na la muhimu ni kuzingatia kuwa mtu huyo awe ni rafiki wa muda mrefu na mtoto ili mtoto asiwe na chembe ya wasiwasi kwamba 'siri yao' inaweza kuwafikia wazazi wake.

## NA KHAMIS KIDAGO 0657 207168

## QUIZ







1. Tuseme umewasili kwenye hoteli moja nchini Ufaransa; ungependa kupata vitu vitatu. Ni vitu gani hivyo? Utaviona vimefichwa kwenye mkanda wa herufi hapo chini.

   motunechambrepozowiuncafé-moghttunjournaldfc

   i. ......................................

   ii. ......................................

   iii. ......................................

2. Kabla hujaondoka hotelini hapo unataka kununua vitu kadhaa: ungeviulizia vipi kwa lugha ya kifaransa?

   a) Ningependa kununua kadi nne, tafadhali.

   ......................................................................

   b) Una stempu hapa?

   ......................................................................

   c) Na aspirini, tafadhali.
   d) Ni bei gani?

   ......................................................................

3. Oanisha maneno ya upande wa kushoto na yale ya upande wa kulia kupata maana kamili.

   a) Deux bouteilles chewing gum
   b) Un kilo vin
   c) Une boîte de sardines
   d) Un paquet sucre

4. Andika majibu yako kwa hesabu zifuatazo (kwa maneno kwa lugha ya kifaransa, sio tarakimu).

   i. deux + trois =......................................
   ii. cinq +quatre=......................................
   iii. neuf+un=......................................
   iv. six+trois=......................................
   v. dix-huit=......................................
   vi. sept-trois=..............................
   vii. trois×troi=..............................
   viii. quatre×deux=..............................

5. Kama rafiki wa kifaransa akikwambia comment ça va? Utamjibu nini? (Jibu kwa lugha ya kifaransa).

   ......................................................................

6. Unaongea Kiingereza na rafiki yako wa Ufaransa. Anakwambia Parlez plus lentement. Hiyo humaanisha nini kwa Kiswahili?

   ......................................................................

7. Una maumivu ya kichwa. Umefika kwenye duka la dawa:

   - Sema unataka nini kwa kifaransa.

   ......................................................................

   - Mshukuru muuza dawa na mwambie kwaheri kwa kifaransa.

   ......................................................................

## WATOTO

## PAKA RANGI




## CHEKA KIDOGO

Msikie mtoto huyu akimuuliza maswali baba yake.

**Mtoto:** Baba unaweza kumwachia hilo gari lako dada wa kazi akaliendesha?

**Baba:** Siwezi kumwachia gari langu hili aliendeshe ni ghali sana.


**Mtoto:** Je, mnaweza kumwachia chumba chenu dada wa kazi kikiwa wazi na mkaenda kazini?

**Baba:** Haiwezekani kamwe, kuna vitu vya gharama na pia heshima haitakuwepo.

**Mtoto:** unaweza ukampa dada kadi ya ATM yako na namba ya siri ukakuchukulie pesa?

**Baba:** Mtoto una balaa wewe, unataka siku akiiba hii kadi akachukue pesa zote tuwe maskini, sithubutu.

**Mtoto:** aahaaaaaa, kumbe hauwezi kumkabidhi chochote chenye thamani dada wa kazi, sasa kwa nini mnanikabidhi mimi kwake nyie mnaenda kazini mpaka mnarudi, kumbe mimi sina thamani kwenu eeeeh



Alichokifanya daktari

SWALI
Bwawa kubwa la umeme linajengwa wapi katika Mto Rufiji?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Anataka kunipa talaka, nawaza muda niliopoteza kuishi naye

MPENZI msomaji, karibu tena tuendelee na vimbwanga vya Maisha Ndivyo Yalivyo ndani ya familia zetu. Wapo watu wanatamani kuingia kwenye ndoa, lakini wengine wanazikimbia au wako njia panda wakivumilia wasijue cha kufanya.

Wote hao, siyo kwamba hawazitaki bali yale yanayojitokeza baada ya kuingia agano hilo la ndoa. Unapoingia kwenye ndoa inakubidi kujitafakari kama upo tayari au la.

Pia yapo mambo mengi ya kuzingatia kabla, ikiwa ni pamoja na kufanya utafiti kama huyu unayemtaka awe mke au mume wako ni sahihi kwa maisha yako. Na unapofanya yote hayo, ni muhimu sana umshirikishe Mungu katika kuamua.

Katika maandiko yake akasema, "Mtumainie Mungu kwa moyo wako wote, wala usizitegemee akili zako mwenyewe". (Mithali 3:5). Ndio maana hata katika uumbaji, yeye ndiye aliyempatia mwanadamu wa kwanza mke. Hivyo Mungu anahusika katika kukuchagulia. Maisha Ndivyo Yalivyo.

Katika maisha ya ndoa, ipo mitikisiko inayoweza kutokea ikiwa ni pamoja na uchumi wa familia kuyumba, wakwe kumbadilikia mkamwana, ndoa isipokuwa na mtoto, kulalamikiana ushirikina na kadhalika.

Kabla sijaendelea, hebu sikia kinachomsibu mwenzetu mmoja. Wiki iliyopita tuliona baba mmoja akihangaika mkewe amrudie kwa miaka minne bila mfanikio. Walitoka Kigoma kwenda Mwanza, Mume huyu alipotaka warudi Kigoma mkewe akagoma hadi leo. Hivi sasa yuko mbioni kutafuta mwanamke mwingine wa kuishi naye.

Sasa leo, tumsikie mama ambaye ameishi katika ndoa miaka minane, lakini sasa mumewe ameweka kusudio la kumpa talaka kwa sababu ambazo haziko wazi. Ndani ya miaka hiyo, bado hajabahatika kuzaa mtoto.

Kwa maelezo yake bibie anasema hivi;- Yupo kijana mmoja walikutana naye chuo kikuu wakati anachukua digrii ya ualimu. Wakadhamiria kuoana mara baada ya kumaliza chuo na kupata kazi.

Alipomaliza chuo, mama huyu akaajiriwa kuwa mwalimu shule ya sekondari. Akiwa kazini akakutana na jamaa mwingine ambaye pia ni mwalimu wakajenga uhusiano, wakajikuta wanakuwa marafiki wa karibu. Bibie akamsahau kabisa yule kijana wake wa kwanza waliyeahidiana kuoana.

Huyu jamaa wa pili hakupoteza muda akatangaza uchumba na kisha ndoa kubwa ikafanyika. Maisha yakaanza katika mazingira magumu, lakini waliendelea.

Muda siyo mrefu jamaa akanunua magari mawili akayafanya teksi za abiria. Baada ya hapo akanunua kiwanja na kujenga nyumba kubwa nzuri. Yote hayo yalifanyika ndani ya miaka miwili ya ndoa yao.

Walipohamia kwenye nyumba yao, misukosuko ikaanza. Ndugu wa mume wakaanzisha chokochoko za hapa na pale. Hiyo ilitokana na jinsi bwana huyo alivyofanikiwa haraka hata kuweza kupata magari na nyumba nzuri kiasi kile.

Haikuishia hapo, ndugu hao wakaanza kuhoji kwanini mwanamke hazai, wakaanza kumchochea mwanaume amfukuze kama hana uzao. Hata hivyo hakuwasikiliza.

Mpenzi msomaji, baada ya kelele za uzao kuzidi, bibie anasema hivi;- "Nikamwambia mume wangu twende tukapime ijulikane tatizo liko wapi. Tukakubaliana kupima, lakini mume wangu akasema kila mtu akapime kivyake.

"Nilipokwenda kupima, hospitali, tena sehemu mbili tofauti, nikaleta majibu yanayofanana kwamba sina tatizo lolote. Nikamuonyesha mwenzangu. Mume naye alipima, lakini hakuweka wazi majibu yake kwangu. Akaficha."

Mume huyu akaomba uhamisho kwenda kufanya kazi mkoani. Sasa ananiambia kwamba anakusudia kuniacha kwa talaka kwani hataki ndoa tena, Nawaza muda niliopoteza kuishi naye katika ndoa hii.

Laiti ningejua nisingeambatana na huyu, ningemsubiri kijana wangu wa kwanza maisha yangekuwa tofauti", anamaliza kusema bibie huyu.

Naam. Bila shaka msomaji wangu umepata picha ya kile anachopitia mama huyu katika ndoa yake. Katika maisha Mungu ameweka utaratibu. Ipo milango ambayo huifungua ili ukutane na waliobeba baraka zako.

Usipoijua, ukatumia tu akili zako mwenyewe, lazima utapata majuto. Siyo kila mtu ni mumeo au mkeo. Yupo mtu sahihi ambaye unapaswa kuambatana naye. Hivyo unapaswa kuwa makini sana katika kuchagua.

Siyo kila nyumba unapaswa kuingia, chunguza kwanza. Zipo familia ambazo asili yao ni kuoa wake wengi. Katika hawa wapo wanaooa na kuacha. Ukijikuta humo, usishangae kuachwa.

***Msomaji wangu, mengine nikuachie utoe maoni au ushauri wako kwa ndoa hii. Nitumie pia kisa kifupi kwa ujumbe mfupi kile kinachokusibu ili tujadiliane kwenye safu hii. Ukiwa tayari wasiliana nami kupitia 0715268581. Namba hii pia ipo whatsApp. Tukutane wiki ijayo.***

## NAWAZA KWA SAUTI
Na Salome Kitomari



# TFS, TAWA mko wapi msitu, hifadhi vinateketea?

YAPO maswali mengi ya kujiuliza kutokana na kinachoendelea katika msitu wa asili wa Minyughe wenye hekta 264,600 uliozungukwa na vijiji 24, ukiwa na miti ya miyombo na wanyamapori, wilayani Ikungi, mkoani Singida.

Tanzania ina eneo la kilomita za mraba 94,500 sawa na hekta milioni 94.5. Kati ya hizo, takriban hekta milioni 481 ni misitu na misitu matajiwazi.

Kati ya hekta milioni 48 hekta milioni 28.0 ni hifadhi ya maji, ardhi na bioanuai, hekta milioni 20 zilizobaki ni misitu na matajiwazi ambayo uvunaji unaruhusiwa kisheria, misitu hii inajumuisha misitu iliyohifadhiwa kwa ajili ya uvunaji na iliyopo kwenye maeneo ambayo hayajahifadhiwa kisheria.

Kwa mujibu wa Sheria ya misitu sura 323 ya mwaka 2002 hairuhusiwi kuvuna miti katika misitu ya hifadhi ya vyanzo vya maji, ardhioevu na bioanuwai.

Rasilimali ya misitu ina umuhimu mkubwa katika suala la uhifadhi wa mazingira na inakadiriwa kuchangia asilimia mbili hadi tatu kwenye pato la Taifa.

Pia, shughuli mbalimbali zinazofanywa katika maeneo ya misitu huchangia kupunguza umaskini miongoni mwa jamii ya Watanzania, misitu pia ni chanzo muhimu cha nishati kwa kuwa asilimia 95 ya nishati nchini hutokana na mimea.

Tanzania kuna maeneo ya hifadhi ya jamii Wildlife Management Area (WMA), 32 kati yake 16 ndiyo zenye afadhali na nne pekee ndiyo zinakusanya mapato ambayo yananufaisha vijiji na serikali kwa ujumla.

Kwa ujumla msitu wa Minyughe una uoto wa asili, wanyama kama tembo, twiga, kudu, digidigi na wengineo na kisheria uko chini ya Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania (TAWA), Mamlaka ya Misitu Tanzania (TFS) na Halmashauri ya Ikungi.

Kwa sasa kinachoendelea katika msitu huo ni uharibifu mkubwa unaohitaji nguvu ya pamoja baina ya mamlaka zote za serikali, vinginevyo eneo hilo litapotea na kubaki historia.

Halmashauri ya Ikungi imejitahidi sana kuweka ulinzi na kufanya doria za mara kwa mara, lakini kutokana na nguvu kazi na rasilimali fedha kuwa ndogo imeshindwa kukabiliana na kasi ya uharibifu.

Makundi makubwa ya wafugaji wanaingiza mifugo ndani ya msitu, uchomaji mkaa, ukataji wa mbao na kasi ya shughuli nyingine za kibinadamu ni kubwa hali ambayo sasa inatishia uhai wa eneo hilo.

Nguvu ya viongozi wa vijiji 24 kutunza eneo hilo imekua ndogo kutokana na wafugaji kutoka mikoa ya mbali kuleta mifugo na kuanzisha makazi, kiasi cha wanyama waliokuwapo kuhamia maeneo mengine.

Uharibifu ndani ya msitu huo upo kwa aina nne za kuingia bila kibali maalum, kuingia na aina yoyote ya silaha au zana, kuharibu uoto wa asili kwa kukata miti, mkaa, mbao, magogo, magome.

Pia, wafugaji kuweka makazi na wakulima kufanya shughuli za kilimo, kulisha mifugo na uvunaji wa mkaa.

Licha ya faini mbalimbali kuwekwa na Halmashauri, lakini bado haijasaidia hali inayoonyesha kuwa inahitajika nguvu ya mamlaka za juu kama TAWA na TFS.

Mwongozo wa uvunaji endelevu na biashara ya mazao ya misitu yanayovunwa katika misitu asili ulitengenezwa kutokana na sera ya misitu ya mwaka 1998 na sheria ya misitu sura 323 ya maka 2002.

Mapitio ya mwongozo wa 2007 yamefanyika ili kukabiliana na changamoto zinazojitokeza na licha ya kila kitu kusheheni ndani ya mwongozo huo.

Mara kadhaa Halmashauri imekamata watu aliohusika na uharibifu na kuwafikisha katika vyombo vya dola, lakini bado nguvu ya pamoja inahitajika kwa kuwa kila siku zinatungwa mbinu mpya za uharibifu.

Kama ambavyo imewezekana katika WMA ya Burunge, Babati mkoani Manyara, ambayo wananchi aliona changamoto ya uharibifu wa mazingira, uwepo wa wanyamapori na kuamua kuunda umoja wa kutunza eneo hilo.

Kwa sasa kwa mwaka wanapata mapato yatokanayo na watalii na uwekezaji zaidi ya Sh. bilioni mbili kati yake Sh. bilioni moja inagawanywa kwenye vijiji na nyingine inabaki kwa ajili ya uendelezaji wa jumuiya.

Sehemu ya fedha inakwenda TAWA ambayo ndiyo wanaokusanya fedha zote na kuigawia Burunge, kupitia fedha hizo wananchi wamejenga miundombinu ya maji, afya, shule, nyumba za walimu na kusomesha watoto yatima hadi chuo kikuu.

Kwahiyo, yaliyowezekana Burunge yenye vijiji 10 yanawezekana katika vijiji 24 wilayani Ikungi, mkoani Singida, kiasi cha jamii inayozunguka kunufaika zaidi na shughuli zitakazostawisha msitu huo kuliko uharibifu.

HARUSI

# Usiku wa Janeth









Ilikuwa ni shangwe na vigeregere, katika sherehe ya kuagwa Janeth Richard, Ofisa mikopo wa Platinumcredit, iliyofanyika kwenye ukumbi wa Tanzanite Kimara, jijini Dar es Salaam, Agosti 27, 2020. Mwenza wake ni Bariki Mtui, Mhandisi (TAA)

# MITINDO

## INGIA OFISINI KIAFRIKA ZAIDI

# Vazi la kitenge litakupa mwonekano murua



VAZI la kitenge limekuwa maarufu katika nchi za Afrika. Tanzania ni moja ya nchi ambayo watu wake wanapenda kuvaa kutokana na ubora, muundo na rangi zake za kupendeza.

Wabunifu wa mitindo wanafanya kazi kila siku kubuni na kushona aina mbalimbali ya mavazi ili kukidhi soko la wateja wao.

Wengi wa wanamitindo hao wamejikita katika kutengeneza mavazi yanayotokana na vitenge kwa ajili ya kwenda nayo ofisini na sehemu maalum kama kwenye mikutano na makongamano.

**NGUO ZINAZOFAA OFISINI**

Kumbuka nguo za vitenge ni moja ya vazi linaloruhusiwa kwenda nayo ofisini, lakini unashauriwa iwe imeshonwa bila kuwa na ukakasi kama mipasuo mingi, urembo usiochosha kutazama au urefu unaozingatia maadili.

Zingatia vazi lisikupe kero wakati wa kutembea kutokana na kubana sana au kuwa na ukubwa kupita mwili wako.

Wakati wa kuchagua mtindo gani wa kushona, unatakiwa kupata ushauri kwa wataalamu wa mavazi ili upate kitambaa chenye rangi na muonekano mzuri.

Kumbuka wakati wa kuchagua rangi, aina ya ngozi yako ni jambo muhimu kujua kama rangi ya nguo inaendana na kukupa muonekano maridadi.


Vazi la gauni, sketi, shati, suruali au suti ni nzuri zaidi kuwa chaguo la kwanza kwa sababu linakufanya upate muonekano wa Kiafrika zaidi.

Unaweza kunakshia vazi lako kwa kuvaa viatu au mkanda vinavyolingana kwa rangi. Hata hivyo rangi za aina nyingine unaweza kuvaa, lakini hakikisha haiwezi kuletea mabaya mbele ya watu.

UREMBO

CHEKO MURUA

# Raha uwe na meno meupe



MENO ni kiungo muhimu sana ambacho humpatia mtu muonekano mzuri wakati akiwa na furaha au tabasamu pana.

Ndio maana kiungo hiki huweza kuelezea urembo halisi wa mwanamke na humjengea kujiamini mbele za watu.

Ukiwa na meno meupe, tabasamu linakuwa pana na kicheko kinakuwa murua.

**NINI UHARIBU MENO?**

Meno yakiwa na rangi ya manjano, hii inaashiria imeathiriwa na ulaji wa vyakula, vinywaji vya viwandani na upigaji mbaya wa mswaki bila kuzingatia kanuni bora.

Ukiona meno yana rangi ya kahawiya , basi tambua athari hiyo inasababishwa na maji yenye kiwango kikubwa cha madini ya fluoride, matumizi ya sigara, tumbaku na unywaji wa kahawa.

**JINSI YA KUYATUNZA**

Kutokana na umuhimu wake nimeona nikuletee dondoo za kung'arisha meno yako ili uendelee na furaha.

Tumia Baking soda, madini haya yapo kama nga wa soda. Chukua nusu kijiko cha baking soda, kasha pigia mswaki, au weka pamoja na matone kadhaa ya limau.

Madini haya husaidia sana kung'arisha meno.

Hata hivyo, unashauriwa kuwa mwangalifu, kwani haitakiwi kutumia zaidi ya mara tatu kwa wiki.

Maganda ya ndizi za kuiva ni mazuri kutumia kama msasa wa kusugua meno yako. Kitaalam maganda ya ndizi yana madini ya magniziam, potasiam, na manganese, ambayo husaidia kutakatisha meno yako.

Unachotakiwa kufanya, sugua meno kwa maganda ya ndizi, kisha acha kwa dakika 15 kabla hujaendelea kusafisha kwa mswaki. Karoti ni moja ya chakula kinachosaidia kutakatisha meno. Jitahidi kutafuna karoti kwa wingi kila siku kwani husaidia kuyaweka meno katika mng'aro.

Matumizi ya bizari inaonyesha husaidia kutakatisha meno. Tumia mchanganyiko wa juisi ya limau na unga wa binzari kwa kusugulia meno. Limau, unaweza kusugua meno yako kwa kutumia maganda ya limau, au kutumia maji ya limau.

Matumizi ya karafuu pia uboresha muonekano wa meno pamoja na kuondoa harufu ya kinywa. Karafuu pia husaidia kuuwa vijidudu kinywani na kulinda fizi.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Smoothie ya strawberries, ndizi



**Mahitaji:**

VIKOMBE viwili vya matunda ya strawberries zilizogandishwa.

Maziwa ya mtindi yawe mazito nusu kikombe.

Maziwa fresh nusu kikombe.

Ndizi mbivu mbili ndogo au moja kubwa.

**Namna ya kutengeneza**

Andaa matunda yako kwa kuyashasafishwa vizuri na kuweka kwenye chombo kisafi.

Baada ya maandalizi hayo menya ndizi na zikate vipande.

Chukua brenda na weka mchanganyiko wote ndani.

Anza kusaga mchanganiko huu hadi hapo utakapoona umelainika na utakuwa tayari kwa matumizi.

Mimina kwenye chombo kisafi tayari kwa kuanza kutumiwa.

Unaweza kuweka kwenye jokofu kwa ajili ya kupata baridi na baada ya hapo tayari kwa kunywa.

Unawezwa kunywa kinywaji hiki asubuhi unapoamka kabla hujala chochote, mchana baada ya kupata mlo au usiku kabla ya kulala.

MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya

# Samani huongeza mvuto wa nyumba

HAKIKA nyumba isiyo na samani, haijatimia. Baada ya kumaliza safari ndefu ya ujenzi wa nyumba kwa chaguo analotaka anayejengewa, sasa ni wakati wa kuingia katika hatua nyingine ya kununua vikorombwezo vya kupendeshesha nyumba yako.

Sekta hii pia inahitaji utalaamu na ushauri. Unaweza kuwa na nyumba nzuri yenye mvuto kwa nje, lakini unapoingia ndani thamani ya nyumba ikashuka kutokana samani ulizopangilia.

Japokuwa ni uamuzi wa mtu mwenyewe, pia Msanifu wa Majengo, Simon Mpyanga, anashauri kwamba ili kuendelea kutunza ubora wa nyumba, kuna umuhimu wa kushauriwa na mtaalamu ni aina gani ya samani inafaa, kabla ya kuinunua.





Mpyanga anasema, kabla ya mkazi au mwenye nyumba kuchukua hatua ya kwenda kununua samani, kuna hitaji la ushauri kutoka kwa mtaalamu. Hapo inaelezwa ni vyema ukawaona mafundi wazuri wa samani wanaoeleweka badala ya kutumia 'wajanja wajanja'.

"Bora umuite fundi aje nyumbani kwako, aangalie eneo ambalo linafaa kukaa samani na alipimie. Fundi mwaminifu na mwenye weledi ni lazima atakushauri, ni bora uepuke kuchukua chukua tu wa mitaani wajanja wajanja," anasema Mpyanga.

Anafafanua kwamba kabla ya mtu kununua samani, basi anatakiwa kwanza kwenda kwa mtaalamu, ambaye atakushauri aina ya samani zinazoendana na namna nyumba yako ilivyokaa ndani.

Jambo la pili, anashauri kununuliwa samani kulingana na mpangilio wa rangi katika nyumba, ili kuhakikisha rangi za samani zinashabihiana na zilizopo nyumbani.

Mtaalamu huyo anasema, samani ziendane na rangi ya vitu vilivyopo ndani ya nyumba, kama vile pazia, zuria na mapambo.

MPANGILIO

# Dondoo muhimu kuandaa meza ya kahawa

1: Angalia sehemu ambayo unaweza kuweka meza yako ndogo kwa ajili ya matumizi ya vinywaji. Hakikisha meza haipo sehemu korofi au kwenye utitiri wa vitu.


2: Kama una uwezo weka meza yenye nakshi, lakini iwe fupi tofauti na ile ya chakula. Juu iwe inavutia pale unapoiangalia ili kuhamasisha zaidi.

3: Chagua rangi sahihi kwako na wageni watakaokutembelea. Usichague inayong'ara sana ili kupendezesha meza yako.

4: Weka trei ya kuweka vikombe vidogo au glasi ya kiasi kwa ajili ya matumizi ya kila siku.

5: Meza aina hii inaweza kuweka pembeni ya sofa au kitanda.




KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2020
SMS - 0621 412 879
JUKWAANI
USIENDE KUNAKO MIKUTANO YA KAMPENI KUFUATA KANGA, BALI FUATA NENO LA MGOMBEA ILI UWAPIME NA UWACHUJE
KAZI SASA KUTAFUTA CHUJIO NA MZANI
NITARAHISISHA SULA LA UBWABWA NA MANDONDO KWA KILA FAMILIA ITAPIGA 'UBECHE' KUTWA MARA TATU
NAOMBA URAISI
KAMUONA ALIYE-CHUKUA NAFASI YAKE BAADA YA YEYE KUKATWA
HUYU ALIFUATA NINI MKUTANONI KAMA SIO KILANGA!
HUNIJUIEEE?!
JAMANI MSINI-CHANE MAKWAPA, KUNA MAISHA BAADA YA UCHAGUZI
WEWE NDO HUNIJUI!
MBONA UNA-JICHEKESHA KAMA CHIZI KAONA JALALA JIPYA!
'MEDULA' INAPITIA VIBWEKA VYA AHADI ZA WAGOMBEA MBALIMBALI
HAPA DAWA YAKE KUJA KIVINGINE NA BARABARA ZA CHINI YA BAHARI
UNANUNUA BURE! NISHAKWAMBIA MWAKA HUU MIMI SIGOMBANII
ULITOSWA
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...MBEA HATUMWI AKASEME...

## HABARI KIMATAIFA

# Wabakaji kuhasiwa Nigeria

**ABUJA, Nigeria**

BUNGE la jimbo la Kaduna nchini Nigeria, wamepitisha adhabu ya kuwahasi wanaume watakaokutwa na hatia ya kubaka watoto walio chini ya umri wa miaka minne.

Hata hivyo, adhabu hiyo itakuwa halali kama Gavana wa jimbo hilo, Nasir Ahmad el-Rufai, atatia saini muswada huo ili kuwa sheria kamili katika jimbo hilo lalo Kaskazini Magharibi.

Awali wabunge aliunga mkono adhabu hiyo ili kudhibiti vitendo vya ubakaji.

Sheria ya Nigeria inatoa adhabu ya kifungo cha miaka 14 au maisha kwa mtu aliyepatikana na hatia, lakini wabunge wana haki ya kutunga adhabu ya tofauti.

Hata hivyo, hali ya unyanyapaa inasababisha waathirika kushindwa kuripoti matukio ya ubakaji na kuna idadi ndogo ya watu waliofikishwa mahakamni.

Mwezi Juni mwaka huu, magavana wa nchi hiyo walitangaza hali ya hatari baada ya kuongezeka kwa vitendo vya ubakaji na unyanyasaji dhidi ya wanawake na watoto.

Tangu mwaka 2015, wakati sheria mpya ilipoanzishwa, watuhumiwa 40 pekee wa ubakaji walishtakiwa, takwimu hiyo kulingana na wakala wa Kitaifa wa kuzuia usafirishaji haramu wa watu

**(NAPTIP).**



Alexandra Hamatie, ambaye mpwa wake Robert Horohoe, aliuawa katika tukio la kigaidi la Septemba 11, wakati wa kukumbuka shambulio hilo lililotokea miaka 18 iliyopita.**(PICHA: AFP)**

# Taliban, serikali waanza mazungumzo ya amani

**DOHA, Qatar**

SERIKALI ya Afghanistan na wanamgambo wa Taliban, jana wameanza mazungumzo ya kuleta amani nchini humo.

Wajumbe wa kila upande walijadili hatua za kumaliza vita vilivyodumu kwa muda wa miaka 40 na kusababisha watu wengi kufa na wengine kujeruhiwa.

Mkuu wa ujumbe wa serikali ya Afghanistan, Abdullah Abdullah, katika ufunguzi wa mazungumzo hayo alisema lengo lao ni kumaliza miaka 40 ya umwagikaji wa damu.

, "Tumekuja hapa kwa nia njema na lengo zuri la kusitisha umwagikaji wa damu na kupata amani ya kudumu nchi nzima," alisema Abdullah.

Kiongozi wa ujumbe wa Taliban, Mullah Abdul Ghani Baradar, aliahidi kundi lake litashiriki mchakato huo wa kutafuta amani kwa uaminifu, lakini kuwe na subira.

Baradar, alisema kundi lake linalenga kuwapo kwa Afghanistan ya Kiislamu ambayo itakuwa na uhusiano mzuri na nchi zingine katika kanda hiyo na nchi jirani.

"Mchakato wa mazungumzo bila shaka utakuwa na matatizo, tunauhakikishia ulimwengu kwamba tutajaribu kupata matokeo mazuri," alisema Baradar.

**DW.**

# Watu 50 wahofiwa kufa DRC

**KINSHASA, DRC**

WATU 50 wahofiwa kufa baada ya mgodi wa dhahabu kuporomoka mashariki mwa Jamhuri wa Kidemokrasia ya Congo.

Tukio hilo limetokea juzi katika eneo la machimbo ya Kamituga katika jimbo la Kivu ya Kusini. Ilielezwa maporomoko hayo yalisababishwa na mvua kubwa iliyonyesha katika eneo hilo.

Hata hivyo, Gavana wa Jimbo hilo, Theo Ngwabidje, alisema idadi ya waliokufa ilifikia 50, Meya wa mji wa Kamituga, Alexandre Bundya, anapinga akisema bado hakuna uhakika ya idadi kamili ya watu waliokufa.

**DW.**

# Iran yashutumu Bahrain, Israel

**TEHRAN, Iran**

IRAN imelaani uamuzi wa nchi ya Bahrain kuanzisha uhusiano wa kidiplomasia na Israel.

Kauli hiyo imekuja baada ya Marekani kutangaza mpango huo wa Bahrain, ikiwa ni wiki nne baada ya nchi nyingine ya Umoja wa Falme za Kiarabu, kuanzisha uhusiano wa kibalozi na nchi hiyo.

Katika taarifa yake kwa vyombo vya habari, Wizara ya Mambo ya Nje ya Iran, ilisema "Ni uamuzi wa aibu na mbaya ambao utaingia katika rekodi za vitendo vya kashfa."

Wizara hiyo imeishutumu Israel kwa kuyaweka rehani maumivu ya muda mrefu ya Wapalestina kwa nia ya kumfanyia kampeni Rais Donald Trump ili arudi tena madarakani.

**DW.**

# Peru waanza mchakato wa kumng'oa Rais

**LIMA, Peru**

BUNGE la Peru limepiga mchakato wa upigaji kura ya kutokuwa na imani na Rais wa nchi hiyo, Martin Vizcarra.

Mchakato huo ambao ulianza jana, ukikamilika Bunge hilo linaweza kumng'oa madarakani baada ya kutuhumiwa kwa kosa la kutokuwa na maadili.

Kwa mujibu wa gazeti la Comercio, mchakato wa kupiga kura ukikamilika, inafuatia hatua nyingine ya kumfungulia mashtaka .

Katika hatua ya awali wabunge 65 walipiga kura ya ndio na 36 walikataa, huku wengine 24 hawakushiriki.

Vizcara anatuhumiwa kuwaelekeza washauri wake kufanya udanganyifu katika uchunguzi ulioendeshwa na bunge.

Hata hivyo, Rais huyo aliita hatua hiyo kuwa ni njama dhidi ya demokrasia.

## MAKALA

# Tabia za wagombea wakati wa uchaguzi



Na Magabilo Masambu

MCHAKATO wa wagombea kuendelea kunadi sera za vyama vyao ambazo zinaongozwa na ilani zao za uchaguzi, unaendelea sasa na utakoma Oktoba 28, utakapofanyika uchaguzi mkuu wa kumpata Rais wa Tanzania na wa Zanzibar, wabunge, wawakilishi na madiwani.

Mchakato huu ni kwa mujibu wa Katiba na sheria za nchi. Ibara ya 76(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inasema: "Kila mara baada ya bunge kuvunjwa, kutakuwa na uchaguzi wa wabunge katika majimbo yote ya uchaguzi." Uchaguzi huo unakwenda sambamba na ule wa Rais kwa Tanzania na wa Rais na wawakilishi kwa Zanzibar.

Pamoja na matakwa ya kikatiba na kisheria, jambo mojawapo kwa nini kampeni zifanyike ni kutaka kuwapa nafasi wananchi ambao ni wapigakura kusikiliza sera za vyama mbalimbali ili kufanya uamuzi sahihi siku ya kupiga kura.

Sambamba na wagombea na vyama kujinadi watafanya hivi na vile, pamekuwapo na utaratibu wa baadhi ya wagombea kujaribu kuonyesha tabia ambazo si zao kiuhalisia.

Wagombea wengi wamejaribu kuonyesha maisha ya unyenyekevu ambayo si yao, upendo ambao si wao. Wanafanya shughuli ambazo wakiwa nyumbani kwao hawazifanyi. Yote hayo ni kujaribu kumshawishi mpigakura awaonee huruma na kuwachagua.

Wanafanya hivyo kwa sababu wanaifahamu vyema nguvu ya wananchi katika kuwaweka na kuwatoa madarakani viongozi kupitia sanduku la kura.

Ibara ya 8(1) ya Katiba inasema: "Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi inayofuata misingi ya demokrasia na haki ya kijamii. Kifungu (a) cha katiba kinasisitiza kuwa wananchi ndio msingi wa mamlaka yote, na serikali itapata madaraka na mamlaka yake yote kutoka kwa wananchi.

Sina hakika kama wananchi wa Tanzania tunafahamu nguvu tuliyo nayo kikatiba katika kuwaweka na kuwatoa viongozi kupitia sanduku la kura. Nguvu hii ndiyo inayowapa hofu wagombea kwamba wananchi wakiamua, wanaweza kuitumia kumtoa yeyote na kumuweka yeyote. Wagombea kwa kulifahamu hili, hufanya maigizo mengi vipindi vya uchaguzi. Baada ya kushinda, tabia zao halisi hujulikana waziwazi.

Tabia za namna hii nyakati za uchaguzi, nyakati zingine hazionekani. Wagombea wanafanya hivyo kwa kuwadharau wananchi na kuwaona hawajui lolote. Wananchi wanapaswa kutodanganyika na maigizo ya namna hii. Wanayeshirikiana naye siku zote anajulikana, anayefanya haya kwa ajili ya uchaguzi tu anajulikana pia.

Vipindi hivi vya uchaguzi ni inapaswa kuwa makini sana kutofanya makosa ya siku moja ya uchaguzi majuto yakaishi miaka mitano. Wananchi wachague watu wanaojua watawaongoza katika kutatua kero zao.

Wagombea hawana sababu ya kuyafanya hayo kama si sehemu ya maisha yao. Kama wanatamani wananchi wawapende kwa kushiriki kwenye shughuli zao, wafanye haya kila wakati na iwe utamaduni na sehemu ya maisha yao. Uongozi usimfanye mtu kuwa mbali na wananchi na kutamani kuwa nao karibu wakati wa uchaguzi. Tabia za baadhi ya wagombea zinazoonekana nyakati za uchaguzi, zingelikuwa tabia zao halisi, kungekuwa na taifa bora sana. Kusingekuwa na viongozi walio mbali na wananchi mpaka kujiuliza ndiye Yule aliyekuwa akichambua mpaka dagaa au kujitwisha ndoo za maji kichwani?

Faida kubwa ya wagombea kufanya tabia za nyakati za uchaguzi kuwa tabia zao za kudumu ni huepusha kutumia nguvu kubwa na rushwa kushinda uchaguzi kwa sababu wananchi hawa hawahitaji mambo makubwa sana ukiwa sehemu ya maisha yao. Watakuwa walinzi wako, wasemaji wako, hutawahonga chochote kwani watakuona ni mwenzao.

Maigizo haya hufanywa hata na wale ambao wameshakuwa madarakani. Mtu amekuwa mbunge miaka mitano, hajawahi kufanya mkutano wowote wala kuonekana jimboni, lakini ukifika uchaguzi anakuja kuchambua mchele na kinamama. Kwa nini usiwe unachambua siku zote unapokuwa mbunge?

Wapo wanaokimbia majimboni kwa kuogopa kero za wananchi. Sasa kama unakimbia kero unaomba tena kuongoza kero wa wananchi wako zimeisha? Unapoomba uongozi maana yake unataka kushirikiana na wananchi kujiletea maendeleo.

Ni vyema mtu anapogombea badala ya kusema atafanya au kutoa kitu fulani, aonyeshe kwamba atashirikiana na wananchi ili wajiletee maendeleo. Kazi ya kiongozi ni kuwapa dira na si kuleta hiki au kile. Mtu akisema ataleta au kufanya kile hiyo ni ahadi na siku zote ahadi ni deni na ni lazima aliyeahidi alipe. Mfumo wa maisha ya kuigiza umeharibu mambo mengi na hili si Tanzania tu wala si viongozi tu. Hata katika maeneo mengine, tabia za kujikweza zimetufanya tuishi maisha yasio yetu. Haya yanaweza kuonekana mambo madogo lakini hata mbuyu ulianza kama mchicha!

Sifa moja kubwa ya kiongozi bora ni uwezo wa kusikiliza watu si wakati wa uchaguzi tu bali hata baada ya kuchaguliwa. Viongozi wengi huwa mbogo pindi wakishachaguliwa. Suala si kuwa mpole kwa watenda maovu bali kuwa mtu anayeweza kufikika kirahisi na wananchi kwani ndio wanaomwajiri. Si vyema kuwanyenyekea wananchi wakati wa uchaguzi lakini baada ya kupata madaraka, unaota mapembe. Hata kuonekana unakuwa kama kakakuona! Wengine mpaka hutoa maelekezo kwa wasaidizi wao kwamba "watu wakija waambie sipo au nina kikao" lakini wakati wa kuomba kura ulikuwa na muda wa kutosha mpaka wa kuteka maji kisimani.

Ni vyema wagombea wakaziishi tabia wanazozionyesha sasa. Kwa kufanya hivyo, hawatakuwa na haja ya kutumia rushwa ili wachaguliwe. Wananchi pia watambue kuwa mtu anayetoa rushwa na kushinda, cha kwanza atahakikisha anarudisha fedha alizotumia badala ya kuleta maendeleo. Mtu anayepokea rushwa pia atambue kuwa atajutia rushwa hiyo kwa miaka mitano.

Mungu ibariki Tanzania, Mungu ibariki Afrika

**Kwa maoni na ushauri**
**068915778 magabilomjalifu@gmail.com**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Vituko vya Drive Inn Cinema Dar



Na Adam Fungamwango

JAMAA mmoja alikuwa sebuleni na watoto wake. Walikuwa wakiangalia filamu huku watoto na mkewe wakifurahia hali hiyo. Lakini mkewe aligundua kuwa mumewe kama vile anawaza kitu.

Akamuuliza kwa nini ana mawazo sana. Akamwambia kuwa wakati akiwa mdogo hali kama hiyo ya kuangalia filamu sebuleni ilikuwa haiwezekani.

Alimwambia wakati akiwa mdogo wa miaka minane mpaka kijana wa miaka 20, ilikuwa haiwezekani filamu kuangalia nyumbani badala yake yeye na vijana wenzake, walikuwa wanafunga safari kwenda kwenye kumbi mbalimbali za sinema.

Akamwambia mkewe na watoto wake kuwa wakati mwingine hata kukata tiketi ilikuwa shida. Ilikuwa lazima uwe na ubavu ndiyo upate tiketi. Pia kulikuwa na tiketi za magendo.

"Kweli hivi sasa kuna maendeleo, yaani imefika wakati hata sinema ambazo sisi tulikuwa tunazipatia tabu kwenda kuziangalia leo naziangalia sebuleni kwangu.

Ama kweli hii ni dunia ya teknolojia. Pamoja na kwamba mkewe na watoto wake walikuwa wakimshangaa kwa maneno yake, alikuwa sahihi.

Miaka ya 1980 mwanzoni hadi 1990 mwanzoni, vijana waliozaliwa au kuishi Dar es Salaam wakati huo, watakumbuka kulivyokuwa na kumbi mbalimbali za starehe za muziki na sinema.

Leo tutaangalia kumbi za sinema ambazo zilitingisha sana wakati ule na vituko vyake.

Watoto, vijana na hata watu wazima wa wakati huo, wakitaka burudani ya kuangalia filamu, wakati huo zikiitwa 'picha', ni lazima waende kwenye kumbi ambazo ni maalum kwa kuonyesha sinema mbalimbali za kizungu, kichina na kihindi.

Kwa asilimia kubwa, watoto na vijana wa wakati huo walipendelea sana picha za kibabe.

Kumbi zilizotamba jijini Dar es Salaam ni Cameo, Odeon, New Chox, Avalon, Empress, Empire, Star Light na Drive Inn ambao watoto wa mjini waliuita 'Drai'. Huu ndiyo ukumbi maarufu zaidi wa sinema jijini Dar es Salaam kwa sababu haikuhitaji kuwa na kiingilio ili kwenda kutazama picha bali uwezo wa kutembea tu kutoka unakoishi hadi hapo.

Kwa vijana wa sasa, Drive Inn Cinema ni maeneo ya Msasani, ambapo kwa sasa kuna Ubalozi za Marekani. 'Drai' ilijengwa tofauti na kumbi zingine zote, nadhani nchini Tanzania.

Wakati kumbi zingine zilijengwa kama majumba ya starehe ambayo ni lazima ukate tiketi na kuingia ndani, 'Drai' ilijengwa kama vile uwanja wa mpira, tena vile vya mikoani, au Uwanja wa Uhuru. Na hata ukubwa wake unafanana na viwanja hivyo.

Lakini kulikuwa na ukuta mkubwa pembeni juu, kama vile jukwaa ambalo lilitumika kuonyeshea sinema. Wakati huo hata ukiwa maeneo ya Kinondoni, Makumbusho na Kijitonyama, ukuta ule au 'bodi' la sinema, lilikuwa kinaonekana vizuri tu.

Kulikuwa na watu wa aina mbili waliokuwa wakitazama sinema maeneo ya Drive Inn.

Ulijengwa maalum kwa watu kwenda na magari na familia zao ambao walikuwa wakiingia ndani ya uwanja kupitia magetini na humo ndani kulikuwa na maeneo maalum ya kukaa watu na familia zao pamoja na sehemu za kupaki magari yao. Na ndiyo maana ukaitwa 'Drive Inn'.

Aina nyingine ni wenzangu na mimi. Hawa ndio walikuwa wengi zaidi kuliko waliokuwa wanaingia na kulipa kwa pesa.

Walikuwa wakikaa nje ya uwanja au ukumbi huo, lakini walikuwa na uwezo wa kuangalia sinema vizuri tu. Tatizo lilikuwa moja. Watu waliokuwa nje ambao wote hawakuwa wanalipa, yaani bure kabisa, walikuwa hawasikii sauti. Sauti ziliishia ndani kwa wale waliongia na magari yao.

Iliaminika kuwa waliokuwa wakiingia ndani mle na magari yao ni watu wenye uwezo tu, mabalozi, wakurugenzi, mameneja, wafanyabiashara wakubwa na watu wengine wenye pesa zao.

Sasa wale watoto wa uswahilini, Kinondoni, Mwananyamala, Magomeni, Msasani, Mburahati, Kigogo na wakati mwingine watu wazima, walikuwa wakijazana nje na kuangalia picha na ilikuwa kuanzia saa 12 jioni wakati mwingine hadi saa nne usiku au tano.

Taabu nyingine ilikuwa mbu kwa sababu ilikuwa nje na pembeni kulikuwa na majani mengi. Kulikuwa na mbu wengi kiasi cha watu kusema 'Drai tiketi ni mbu,' wakiwa na maana sehemu ile haikuwa na kiingilio, lakini lazima uvumilie mbu.

Ni sehemu ambayo ilivuta wafanyabiashara wengi wa vyakula vidogo vidogo, kama 'ice cream', vinywaji na vitafunwa.

Sinema zilizokuwa zikitamba wakati huo ni zile za Bruce Lee, War Bus, American Ninja, Snake In The Monkey Shadow na nyingine nyingi, huku za kihinda ni 'Loha', 'Nasseb', 'Disco Dancer', 'Dance Dance', 'Andha Kanoon,'Hatya' na zingine nyingi.


Kuna baadhi ya watu ambao walikuwa wakiangalia sinema hizo kibubububu nje ya 'Drai', lakini wakirejea nyumbani wanakuwa wasimuliaji wazuri na watafsiri kwa wenzao.

Cha ajabu ni kwamba licha tu ya kutojua lugha ya Kiingereza au Kihindi, hata sauti walikuwa hawasikii, walikuwa wakisimulia picha ilivyokuwa utadhani wao ndiyo watunzi wa hiyo sinema.

# HADITHI

DUNIA ina mambo mengine ya kushangaza. Unaweza kukuta baadhi ya mtu au watu wanaacha shughuli zao na kufuatilia ya wenzao, hata kama hawalipwi. Wanatumia muda mwingi kusema ya wenzao, huku yao wakiwashinda. Wengine ni watu wa karibu kabisa. Tatu, baada ya kuolea na Rashid, yanamkuta ya kumkuta kutoka kwa mama mkwe wake, pamoja na jirani yake Zubeda. Alitamani ardhi ipasuke ajifukie chini. Fuatilia kisa hiki cha kushangaza.

# Mama Mkwe- 2



MATESO yaliendelea kumuandama Tatu. Siku mbili zingine baadaye akiwa bombani, alikutana na Zubeda.

Kila mmoja alikwenda kivyake kuchota maji. Hakuna aliyeongea na mwenzake. Zubeda, baada ya kujaza maji yake, alijifanya anajitwisha, lakini anashindwa na kumwagia Tatu maji. Tatu alilowa, lakini hakusema kitu.

Wakati baadhi ya akinamama bombani hapo wakidhani kuwa ilikuwa ni bahati mbaya, walisikia sauti iliyoashiria shari. "Haya kwamwambie yoyote unayemtegemea kama mimi nimekumwagia maji."

Zubeda alitoa maneno hayo huku akiwa amejitwisha ndoo na kuondoka kwa namna ambayo ilionyesha kuwa ni mshari.

Akinamama na akinadada bombani hapo walishangaa na kukasirishwa na kitendo hicho, lakini hawakuwa na la kufanya. Baadhi walimfariji Tatu, kwani kuna waliokuwa akilifahamu 'bifu' la Tatu, mama mkwe wake na Zubeda.

"Hivi hii dunia tunakwenda wapi?" Alisikika mama mmoja bombani hapo. "Binadamu tumekuwa na roho ngumu kiasi hiki?"

"Tukio alilofanya Zubeda kusema kweli mimi sijalipenda, inafikia steji anamwagia mwenzake maji tena mbele za watu, lo!" Msichana mmoja alisikika mara baada ya Tatu kuondoka, akiwa amebeba ndoo yake kichwani, lakini pia akiwa ameloa kwa kuwamwagiwa maji.

Wakati huo, Zubeda alikuwa amewahi nyumbani kutua ndoo na akaenda kwa mashoga zake jirani kupiga umbeya.

Kwa mbali alionekana Tatu akiwa na ndoo yake ya maji. Zubeda akiwa na wanawake wenzake watatu walipomuona walianza kucheka kiumbea.

"Heheee, jamani kisalata wa mtaa asiyejua vibaya huyoo anapita." Mmoja wa mashoga zake Zubeda alilianzisha.

"Heheee, wadudu wadogo wadogo, wananyevuanyevua." Zubeda yeye naye alicheka, ikiwa ni kumuunga mkono mnafiki mwenzake.

"Na ungekuwa na nyama wewe, hii dunia tusingeikanyaga." Dada wa mwanzo alirudia tena.

"Na ile mirasta kama mwendawazimu, umeiona? ila weupe nao unakustiri shoga, vinginevyo ungekuwa kama kinyago cha mpapure" Msichana mwingine ambaye akadakia, kisha akaendelea.

"Rashid kapotea njia, nilimwambia nioe mimi, akaenda kukuchukua kinyago kama wewe, sijui alikupendea nini na dera waachie wenye shepu

"Tukio alilofanya Zubeda kusema kweli mimi sijalipenda, inafikia steji anamwagia mwenzake maji tena mbele za watu, lo!" Msichana mmoja alisikika mara baada ya Tatu kuondoka, akiwa amebeba ndoo yake kichwani, lakini pia akiwa ameloa kwa kuwamwagiwa maji. Wakati huo, Zubeda alikuwa amewahi nyumbani kutua ndoo na akaenda kwa mashoga zake jirani kupiga umbeya.

zao dada we kha!".

Hadi Tatu alipokuwa hasikii kabisa mazungumzo yao, lakini alikuwa ameyakoga maneno ya kifedhuli kutoka kwa Zubeda na shoga zake ambao walikuwa wakikaa makusudi kimkakati kwa ajili ya kuchokonoa tu.

******************************

"Mume wangu, mimi naona kama dunia hii yote imenielemea, Kuolewa na wewe naona kama nimeolewa na dunia nzima. Sina raha. Afadhali ingekuwa sina raha sehemu moja tu, lakini mama mkwe tatizo, majirani tatizo na hata njiani nikipita tatizo, nachekwa, nasakamwa, naambiwa maneno mengi, nabezwa, kisa sikielewi." Tatu alikuwa amekaa kwenye mkeka sebuleni, akiwa anasuka ukili, huku mumewe akiwa amekaa kwenye kiti chenye mbao na sponji zilizochakaa ambacho zamani kilitwa kochi.

"Kwani tatizo hulielewi mke wangu? Sisi tunapendana sana, ndiyo maana watu wengi hawapendi hili, hata mama yangu pia anajazwa na maneno ya majirani." Rashid alianza kutuliza mkewe.

"Mume wangu, mimi naona kama nimetumbukizwa kwenye shimo kubwa lenye mamba wanaotafuna taratibu au kama nimeibeba dunia zima kichwani."

"Mke wangu, hata mimi ninayekupa faraja hunioni? Ninayekukinga na yote huniangalii?" Rashid aliendelea kumtuliza mkewe ambaye alikuwa akiongea maneno yenye dalili za kukata tamaa.

"Hapana mume wangu, mimi nakupenda sana na nitaendelea kukupenda milele na ipo siku tu, utakuja kuona au kuthibitisha upendo wangu kwako, lakini kwa sasa naona kama kuishi hapa kutanishinda."

Rashid alishtuka maneno ya mwisho kuwa 'kuishi hapa kutanishinda.'

Alimpenda sana mkewe, na mapenzi yao yanaonekana kama kuwakera wengi kijijini hapo, ukichanganya na Bi. Mwapewa na binti yake wa hiari Zubeda ambao wamekuwa wakitangaza kuwa Tatu ametoka katika familia ya wachawi na amempa dawa ya mapenzi, maarufu kama limbwata mumewe, ndiyo maana amekuwa akimpenda kupita kiasi, akifanya chochote kwa ajili ya mkewe.

"Hapana mke wangu, tuombe Mungu, yote haya yataisha." Rashid bado aliendelea kusihi mkewe.

"Hapana, mimi nadhani mama yako anaona utapata mwanamke mwingine mzuri kushinda mimi, maana mimi siyo wa kunyoonyewa vidole kila siku." Alisema na kuanza kuangia kilio.

Rashid akawa na kazi ya kumbembeleza mkewe.

"Sasa mimi nasema hivi mume wangu, hata kama bado hatuna maisha mazuri, hata kama hatuna pesa za kutosha kama unataka niendelee kuwa na wewe, basi tuhame hapa kwenu, twende tukakae mbali na mama yako, mbali na watu wa hapa." Aliongea kwa kigugumizi.

Kuhama hakukuwa shida kwa Rashid, lakini tatizo kubwa lilikuwa ni pesa. Bado hakuwa na pesa za kutosha za kwenda kupanga, au kujenga nyumba japo ya matope na nyasi.

Hata hivyo aliona maneno ya mkewe yana mantiki. Aliona kabisa akiendelea kukaa pale mke atamkosa.

"Hasa mke wangu, nimekusikia, nipe muda nijipange, nitafanya mawili, ama nitajenga nyumba kwanza ya matope na nyasi ili tuondoke tu kwanza hapa, au tukapange sehemu." Tatu alikubali kwa kichwa maneno ya mumewe.

******************************

Wiki moja baadaye Tatu alitembelewa na dada yake Salima. Ilibidi mdogo wake ampe ubuyu wote uliokuwepo pale.

"Yaani dada nimetengwa wenzio, naambiwa namtesa kaka yao, sijui nimempa limbwata, namfulisha minguo, nampikisha mimi, yaani hapa nilipo nipo hoi kama mbwa koko. Kila ninapopitwa nakodolewa macho. Nimechoka kabisa kuishi hapa, nimemwambia mume wangu, atafute pesa kijiji hiki tuhame, twende popote pale mimi niko radhi, vinginevyo mimi niache tu nirudi kwetu."

"We mdogo wangu naye mkimya sana. Mpole sana." Salima alilianzisha kwa sauti ya ukali kidogo kama kwamba anamwambia mtu wa nje, kumbe anaye mle mle ndani.

"Ingekuwa mimi thubutu, ningegaragazana nao kwenye majani, si unanijua mimi vizuri." Alisema Salima huku akisimama na kutoka ndani ya chumba cha mdogo wake kwa nguvu.

Barazani alimkuta Bi.Mwapewa kama kawaida akiwa na binti yake wa hiari Zubeda.

INAENDELEA JUMAPILI



# ATESEKA

## Meneja wa Aslay asema ukimya wamponza

MSANII nyota wa Bongo Fleva, Aslay, anateswa na taarifa za kuzushiwa mabaya ikiwamo kifo, na kusababisha akose raha.

Meneja wa msanii hiyo, Chambuso, amejitokeza na kusema Aslay, ana tabia ya ukimya jambo lililosababisha wabaya wake kupata nafasi ya kumzushia mabalaa kila kukicha.

Akizungumza na EATV, amesema kuwa msanii sio mtu wa kujibu na kutumia mitandao ya kijamii ndiyo maana watu wanamzushia vitu vingi kama hivi sasa walivyoripoti amefariki.

Alisema walikuwa na wakati mgumu wakati taarifa hizo zikisambaa mitandaoni, kiasi ambacho ilibidi kurudi haraka jijini Dar es Salaam, kuweka sawa hali ya hewa.

"Aslay aliamua kukaa kimya kuanzia kwenye mitandao akawa haposti kitu na huwa hamjibu mtu, hili likaleta watu kumzushia kifo, ila ukweli ni kwamba Aslay yupo hai," amesema.

Akaongeza kusema "Kwa hiyo tulichofanya ni kutoa taarifa polisi ila ubaya watu wanaoimiliki hiyo akaunti ya YouTube, hawajulikani na tumewashtaki kwenye mtandao huo kwahiyo baada ya wiki 2 zitashushwa zile taarifa"

Aidha Chambuso, amesema mashabiki wa mwanamuziki huyo watarajie kuona uzinduzi wa Albam yake utakaofanyika baada ya uchaguzi mkuu.

# Country Boy neema tupu Konde Gang

BAADA ya wanamuziki wa Bongo Fleva, Killy na Cheed kujiunga na Konde Gang, mapema wiki hii, sasa ni zamu ya rapa Country Boy, kutambulishwa rasmi.

Kiongozi wa lebo hiyo, Harmonize, jana ametangaza kumsainisha mwanaHipHop huyo na kufikisha wasanii sita.

Licha ya kuwatambulisha wasanii hao, aliwafanyia 'sapraizi' Country Boy na Ibraah Tz kwa kuwapa gari aina ya Crown kwa kila mmoja.

Wasanii wanaomilikiwa na lebo hiyo ni Ibraah, Young Skales, Killy Cheed pamoja na Country Boy




# Hamis BSS hana bahati tu

MSANII aliyejipatia umaarufu kwenye mashindano ya kusaka vipaji vya kuimba ya Bongo Star Search (BSS), Hamis, amekana kwamba alitaka pesa nyingi ili kujiunga na lebo ya Konde Gang.

Akizungumza kwenye shoo ya Friday Night Live, inayorushwa na EATV, Hamis, amesema si kweli alihitaji pesa nyingi ili kujiunga lebo hiyo iliyo chini ya Harmonize, kwani yote yanayotokea ni mapenzi ya Mungu.

"Si kweli kwamba nilihitaji pesa nyingi kujiunga na Konde Gang, ila ni riziki tu Mungu anatoa kwa kila mtu, mimi kiukweli nimefurahi kwa wasanii waliotambulishwa, Naamini Mungu tu anafanikisha kwa kila mtu kwa wakati wake ila kwa kawaida natamani ningekuwa mimi" amesema Hamis BSS



# United sasa yaamua kuachana na Sancho

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United ipo tayari kuachana na mpango wa kumsajili nyota wa Borussia Dortmund, Jadon Sancho, kwa mujibu wa gazeti la Daily Star.

Sancho amekuwa akihusishwa sana na mpango wa kuondoka kule Dortmund na Man United ndio inayotajwa kupewa nafasi kubwa ya kumsajili.

Lakini mchezaji huyo wa kimataifa wa England bado amebaki nchini Ujerumani na United sasa inaonekana kutokuwa na nafasi tena ya kumsajili.

Sancho mwenyewe ameonyesha nia ya kutaka kuondoka, lakini United bado haijafikia makubaliano na Dortmund kuhusu bei ya kumnunua mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20.

Wakati United na Dortmund wakiwa bado wanajadiliana kuhusu thamani ya Sancho, 'Mashetani Wekundu' hao wanaonekana kutokuwa kwenye nafasi ya kuipata saini yake.

Na sasa nyota wa Juventus, Douglas Costa, Joao Felix wa Atletico Madrid na Gareth Bale wa Real Madrid ndio wanaoonekana kuwaniwa na United.





# GATTUSO ATOA MSIMAMO WA KOULIBALY KUTUA CITY

**NAPLES,** Italia

KOCHA Mkuu wa Napoli, Gennaro Gattuso, amesema Kalidou Koulibaly atabaki kama bei iliyotajwa na klabu hiyo ya Serie A haitafikiwa na Manchester City inayoripotiwa kumuwania mlinzi huyo.

Koulibaly amekuwa akuhusishwa sana na miamba hao wa Ligi Kuu ya England, City, ambao inaaminika wanaandaa ofa kwa nyota huyo wa kimataifa wa Senegal.

Manchester United na mabingwa wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, Paris Saint-Germain pia nazo zimetajwa kumuwania.

Hata hivyo, Gattuso ameiambia Sky Sport Italia: "Koulibaly ana bei yake iliyowekwa na kama klabu itashindwa kuifikia, hataweza kuondoka."

Gattuso alikuwa akizungumza Ijumaa baada ya mchezo wa kirafiki walioibuka na ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Pescara huku mshambuliaji Arkadiusz Milik akikosekana.

Roma wameripotiwa kuwa kwenye mbio za kuwania kumsajili Milik, ambaye mkataba wake unamalizika mwaka 2021 wakati Napoli wakiangalia uwezekano wa kumuuza raia huyo wa Poland ili kuepuka kumuacha aondoke akiwa huru.

Mabingwa wa Serie A, Juventus na Tottenham wamekuwa pia wakihusishwa na Gattuso amerudia kamba Milik lazima aondoke baada ya ujio wa Victor Osimhen na Andrea Petagna, ambaye alifunga dhidi ya Pescara.

# *Van Gaal aionya Barca kwa Depay*

**AMSTERDAM,** Uholanzi

MEMPHIS Depay ni mchezaji mwenye kipaji, lakini Louis van Gaal ameionya Barcelona kwamba mshambuliaji huyo wa Lyon hataweza kutatua matatizo yao yote.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 27, anawaniwa na miamba hao wa LaLiga, ambako kocha wa zamani wa Uholanzi, Ronald Koeman amechukua mikoba ya kuinoa kutoka kwa Quique Setien.

Baada ya kuwa na wakati mgumu chini ya Van Gaal kule Manchester United, Depay amefufua kipaji chake kule Lyon kwa kufunga na kutoa pasi za mwisho ambapo ana jumla ya mabao 63 katika misimu mitatu aliyokaa pale Groupama.

Lakini Van Gaal, ambaye alimnoa Depay kwenye kikosi cha Uholanzi, amesema Barca hawatakuwa wamepata mchezaji wa daraja la juu kama Lionel Messi au Cristiano Ronaldo.

"Mara zote kutakuwa na swali," alisema akiiambia Tuttomercatoweb. "Depay ni mchezaji anayevutia, hasa akiwa huru kucheza.

"Lakini lazima tukubali kwamba atatakiwa kwanza kuzoea tamaduni ya timu mpya. Na mara zote mwaka wa kwanza unakuwa mgumu. Angalia kwa (Matthijs) de Ligt au Frenkie de Jong.

"Depay ana kipaji, lakini yeye si Messi au Cristiano Ronaldo."



HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# CRESPO ATIA NENO SAKATA MESSI BARCA

## Unatakiwa mchezaji mwenyewe utoe uamuzi wa busara na kuangalia athari yake…

**BARCERONA,** Hispania

LIONEL Messi alihitaji weledi na hekima yake zaidi na si ya baba yake wakati alipotia nia yakutaka kuondoka Barcelona, kwa mujibu wa mchezaji mwenzake wa zamani wa Argentina, Hernan Crespo.

**Baada ya awali kuiambia Barca anataka kuondoka kutokana na kushindwa kubeba taji lolote msimu wa 2019-20, na kutoelewana na bodi ya pale Camp Nou, Messi alibadili uamuzi na kubaki kwa miamba hao wa LaLiga.**

Mkataba wa Messi unamalizika mwakani, huku Barca wakitaka kumbakiza nyota huyo kwenye kikosi chao ambacho kwa sasa kinataka kufumuliwa chini ya kocha mpya, Ronald Koeman, ambaye amechukua nafasi ya Quique Setien.

Lakini Crespo anaamini tatizo hilo lingeweza kuepukwa, wakati akiiambia TyC Sports: "Kwa hali yote ilivyokuwa, suala ni kwamba... kwa heshima zote kwa Jorge Messi, lakini kwa upande wangu naona jambo lile lilimaliza na weledi wa mchezaji mwenyewe.

"Si jambo rahisi kuzungumza na wakala wako, unatakiwa mchezaji mwenyewe utoe uamuzi ya busara na kuangalia athari yake... wakala ni baba yake na hakuwa na uwezo wa kulimaliza lile.

"Ndio mana nasema ilihitajika busara ya mchezaji mwenyewe na si wakala wake."

Barca itaanza kampeni ya Ligi Kuu ya Hispania kwa msimu huu kwa kucheza na Villarreal, Septemba 26, huku pia ikiwa na mechi za kirafiki dhidi ya Gimnastic Tarragona na Girona.

Barca ilikuwa na msimu mbaya 2019-20, wakati walipoachia taji la Ligi Kuu kwa wapinzani wao Real Madrid, huku wakikumbana na kipigo cha mabao 8-2 kutoka kwa Bayern Munich kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya robo fainali.

Mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or, Messi alifunga mabao 25 kwenye LaLiga na 31 katika mashindano yote msimu uliopita.

## ZISIKUPITE

### SARR AWINDWA LIVERPOOL

LIVERPOOL ipo kwenye mbio za kuwania kumsajili mshambuliaji wa Watford na Senegal, Ismaila Sarr mwenye umri wa miaka 22, katika dirisha dogo la Januari. ***(Football Insider)***

### BARCA YAMTAKA BELLERIN

BARCELONA itatoa ofa ya kumchukua kwa mkopo mlinzi wa Arsenal, Hector Bellerin mwenye umri wa miaka 25. ***(Marca - in Spanish)***

### UTD KUACHANA NA SANCHO



KLABU ya Manchester United inafikiria kuachana na mpango wao wa kutaka kumsajili nyota wa Borussia Dortmund na England, Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 20. ***(Star)***

### MENDY KUTUA CHELSEA

GOLIKIPA wa Rennes, Edouard Mendy mwenye umri wa miaka 28, atafanyiwa vipimo vya afya jijini London wiki hii baada ya Chelsea kufikia makubaliano ya kumsajili nyota huyo wa kimataifa wa Senegal. ***(Star)***

### GIROUD ASHANGAA UVUMI

STRAIKA wa Chelsea na Ufaransa, Olivier Giroud mwenye umri wa miaka 33, "alishangazwa" na uvumi wa kumhusisha yeye na Juventus. ***(Telefoot, via Mail)***

### HUDSON-ODOI ANUKIA MKOPO



CHELSEA inafikiria kumtoa kwa mkopo, winga wake, Callum Hudson-Odoi mwenye umri wa miaka 19. ***(90min)***

### TARKOWSKI GHALI KWA MOYES

KOCHA David Moyes amesema West Ham haitafikia bei iliyotajwa na Burnley kwa mlinzi wake, James Tarkowski mwenye umri wa miaka 27. ***(Football London, via Lancs Live)***

### SPURS KUTOMSAJILI MILIK

KLABU ya Tottenham Hotspur inaonekana haitaweza kumsajili straika wa Napoli na Poland, Arkadiusz Milik mwenye umri wa miaka 26, wakati wa dirisha hili la usajili. ***(Sky Sports)***

### ZAHA HAJAPATA OFA



KOCHA wa Crystal Palace, Roy Hodgson, amesema anashangazwa na klabu "kutogonga mlango" kwa kumuwania nyota wao, Wilfried Zaha mwenye umri wa miaka 27 raia wa Ivory Coast. ***(Standard)***

### WEST BROM KWA DEENEY

KLABU ya West Brom ipo kwenye mazungumzo mazuri ya kumsajili straika wa Watford, Troy Deeney mwenye umri wa miaka 32. ***(Football Insider)***

### YAMWANIA MARTINEZ

BRIGHTON imeingia kwenye mbio za kuwania kumsajili golikipa wa Arsenal raia wa Argentina, Emiliano Martinez. Aston Villa pia inawania kumsajili kipa huyo mwenye umri wa miaka 28. ***(Guardian)***

## HABARI MICHEZO

# Mgunda: Sababu vichapo Coastal

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Coastal Union, Juma Mgunda (pichani chini), amesema kukosa utulivu na kutokuwa na muunganiko kwa wachezaji wake, ndiyo sababu ya kupoteza alama sita katika michezo yao miwili ya Ligi Kuu Tanzania Bara waliyocheza hadi sasa.

Coastal juzi ilipoteza mechi ya pili ya ligi mbele ya Azam FC ambayo iliibuka na ushindi wa mabao 2-0 kwenye mchezo uliopigwa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Mgunda alisema amekubali matokeo hayo, huku akifafanua kuwa kukosa utulivu na muunganiko mzuri kumewasababishia kipigo hicho.

Alisema makosa ambayo wanafanya wachezaji wake yamejirudia tena baada ya kufanya hivyo dhidi ya Namungo FC hali iliyosababisha kupoteza alama tatu.

"Makosa yanajirudiarudia, vijana wengi ni wapya ndiyo wanaanza kucheza ligi, tumejiuliza na tumepata majibu, tunaenda kuyafanyia kazi ili mechi zijazo yasijirudie," alisema Mgunda.

Kuhusu baadhi ya nyota wake kuondoka, alisema hakuna athari kubwa katika kikosi chake kwa kuondokewa na wachezaji wake wengi walioenda kujiunga na timu zingine.

"Athari ipo ila si kubwa sana, ukiangalia tumekosa nafasi nyingi kipindi cha kwanza ila utulivu tu, katika dakika 90 wachezaji wangu wamecheza vizuri na mechi kuonekana ya kiufundi zaidi kwa sababu tumecheza na timu nzuri na wachezaji wa pande zote kuonyesha ufundi mkubwa," alisema Mgunda.

Coastal Union ambayo ilikubali kichapo cha bao 1-0 kutoka kwa Namungo FC kwenye mechi ya kwanza ya ufunguzi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, sasa inaburuza mkia katika ligi hiyo.



# TARIMBA AAHIDI KUPAISHA SEKTA MICHEZO KINONDONI

**Na Jumanne Juma**

PAMOJA na mambo mengine mazuri aliyoahidi, Mgombea Ubunge wa Jimbo la Kinondoni kwa tiketi ya CCM, Abbas Tarimba, amedhamiria kutowaangusha vijana na wanamichezo kwa ujumla katika sekta ya michezo endapo watamchagua kuwa mbunge wao katika uchaguzi mkuu Oktoba 28, mwaka huu.

**Tarimba ambaye ni Mkurugenzi wa Uendeshaji wa SportPesa Tanzania, hata kabla ya kujitosa kuwania ubunge wa jimbo hilo, amekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha sekta ya michezo nchini inapiga hatua kwa kusaidia klabu mbalimbali na soka la vijana.**

Akizungumza katika uzinduzi wa kampeni ya kugombea ubunge katika jimbo hilo kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika viwanja vya Biafra, Kinondoni jana, Tarimba alisema endapo atachaguliwa ataachia ngazi nyadhifa yake hiyo ya sasa ili kuwatumikia wananchi kwa weledi zaidi.

"Kwa upande wa sekta ya michezo, nitahakikisha soka la Kinondoni linakua zaidi kwa kuinua soka la vijana kwa sababu ni chanzo cha ajira," alisema.

Aidha, kwa upande wa masuala ya kijamii mbali na soka, alisema anatambua asilimia 60 ya wananchi wa Kinondoni wanakaa kwenye makazi ambayo siyo rasmi, hivyo atatumia ilani ya CCM ambayo inagusa maeneo ya mabondeni na yasiyo rasmi ili kuyarasimisha.

Alisema chama hicho kinataka kuwasaidia wanyonge, hivyo atahakikisha Kinondoni inabadilika ikiwamo Kata ya Hananasifu, Kigogo, Mwananyamala, Tandale, Makumbusho na Mchafukoge.

Tarimba alisema kata hizo zina changamoto ya mto Ng'ombe na Msimbazi, hivyo atahakikisha anashughulikia kurekebisha miundombinu hiyo kwa haraka atakapopewa ridhaa ya kuwa mbunge wa jimbo hilo.

Kuhusu mikopo kwa kina mama, vijana na walemavu, alisema atahakikisha anakwenda kwenye vikao vya maendeleo na kutoa ushawishi kwa Halmashauri ili mikopo iwafikie walengwa.

"Kata ya Hananasif nimethubutu kujenga sekondari, hivyo ndani ya miaka miwili katika kata hii tutajenga shule mbili na kuanzisha kidato cha tano hadi sita ili watoto wetu wapate fursa ya kuendelea na elimu ya juu," alisema Tarimba.

Alisema akichaguliwa hatautumia ubunge kama cheo, bali atautumia kama taasisi kwa kuwashirikisha wasaidizi wake hata akiwa Dodoma.



Mgombea Ubunge wa Jimbo la Kinondoni kwa tiketi ya CCM, Abbas Tarimba (kushoto), akimpongeza msanii Rajabu Abdul Kahali, maarufu Harmonize ama Konde Boy, wakati akitumbuiza kwenye uzinduzi wa kampeni zake katika viwanja vya Biafra, Kinondoni jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Dube amulika Kiatu cha Kagere*

**Na Mwandishi Wetu**

MSHAMBULIAJI mpya wa Azam FC, Mzimbabwe Prince Dube, ameanza kuonyesha hataki utani katika kuhakikisha straika wa Simba, Mnyarwanda Meddie Kagere, hatwai Kiatu cha Dhahabu kwa msimu wa tatu mfululizo.

Kagere ametwaa tuzo hiyo inayotolewa kwa mfungaji bora wa Ligi Kuu Bara, kwa misimu miwili mfululizo akianza na msimu wa 2018/19 na uliomalizika 2019/20, huku mabao yake yakichangia kuibebesha ubingwa timu yake katika misimu hiyo.

Lakini Dube ambaye amesajiliwa na Azam FC msimu huu akitokea Highlanders FC ya Bulawayo, Zimbabwe, juzi usiku aliibebesha timu yake ushindi wa pili mfululizo baada ya kupachika mabao mawili kimyani wakati wakishinda 2-0 dhidi ya Coastal Union ya Tanga kwenye mechi iliyopigwa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi nje kidogo ya jiji la Dar es Salaam.

Dude sasa amehusika katika mabao yote ya Azam FC kwenye ligi hiyo msimu huu kwani katika mchezo wa ufunguzi dhidi ya Polisi Tanzania, alitoa pasi ya mwisho kwa Obrey Chirwa wakati wakishinda 1-0.

Katika mechi hiyo ya juzi, ilishuhudiwa kipa wa Coastal Union, Abubakari Abasi akifanya kazi kubwa ya kuokoa mabao, huku Dube akifunga bao la kwanza dakika ya 69 baada ya kuitendea haki pasi ya winga Iddi Suleiman 'Nado' na la pili akimalizia pasi ya Mzimbabwe mwenzake, kiungo mshambuliaji Never Tigere dakika ya 89.

Bao hilo la pili, sasa ndilo linashikilia rekodi ya kuwa bao la usiku zaidi mpaka sasa kwa msimu huu wa 2020/21, kabla ya mechi za jana, likifuatiwa na la Kelven John wa Biashara United ambalo alifunga dakika ya 88 kwenye mechi ya ufunguzi dhidi ya Gwambina FC katika Uwanja wa Kumbukumbu ya Karume mjini Musoma.

Hata hivyo, Dube na Mzamiru Yassin wa Simba ndio waliopo kileleni katika orodha ya wafungaji vinara kwenye Ligi Kuu hadi sasa, kila mmoja akiwa na mabao mawili, huku Kagere aliyemaliza na mabao 22 msimu wa 2019/20, akiwa bado hajafungua akaunti yake msimu huu.

Lakini pia mabao hayo ya Dube, yaliiweka Azam FC kileleni kwa muda juzi kabla ya jana KMC FC kuichapa Tanzania Prisons 2-1 na kukaa kileleni kwa tofauti kubwa ya mabao ya kufunga na kufungwa.

# Michezo

Jumapili Septemba 13, 2020

Nipashe





Crespo atia neno sakata Messi Barca UKURASA 22

HESABU...




Kiungo mshambuliaji wa Simba, Clatous Chama, akipiga hesabu ya kuwachambua mabeki wa Mtibwa Sugar, Salum Kanoni na mwenzake, wakati wakitoka sare ya bao 1-1 kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Jamhuri mjini Morogoro jana. **PICHA: SOMOE NG'ITU**

# SIMBA YAPALIWA MIWA YA MTIBWA

## Yabanwa mbavu huku Mzamiru akimfuata kileleni Dube wa Azam, KMC nayo haikamatiki...

**Na Somoe Ng'itu,** MOROGORO

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Bara, Simba, wameshindwa kutamba baada ya kulazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Mtibwa Sugar katika mechi ya ligi hiyo iliyochezwa Uwanja wa Jamhuri mkoani hapa jana.

**Kwa matokeo hayo, Simba imefikisha pointi nne kutokana na mchezo wake wa fungua dimba dhidi ya Ihefu FC kushinda mabao 2-1 huku ikishuka hadi nafasi ya nne kwenye msimamo wa ligi hiyo, wakati Mtibwa Sugar yenyewe imefikisha pointi mbili ikiwa nafasi ya nane, kutokana na mechi yake ya kwanza kutoka suluhu na Ruvu Shooting.**

Simba ilienda mapumziko ikiwa mbele kwa bao 1-0, shukrani kwa kiungo wake, Mzamiru Yassin ambaye alifunga bao hilo dakika ya 44 akiwahi mpira miguuni mwa mabeki wa Mtibwa Sugar, hilo likiwa la pili kwake msimu huu.

Katika mchezo wa awali jijini Mbeya kwenye Uwanja wa Sokoine dhidi ya Ihefu FC, Mzamiru alifunga moja na kutengeneza lingine wakati wakishinda 2-1, hivyo kwa mabao hayo anakaa kileleni kwenye orodha ya wafungaji sambamba na Prince Dube wa Azam FC wenye mabao mawili.

Hata hivyo, Mzamiru hakushangilia bao hilo baada ya kufunga na aliamua kunyoosha mikono juu akiashiria kuwaomba radhi waajiri wake wa zamani kutokana na kufunga.

Kipindi cha pili kilianza kwa kasi na Mtibwa Sugar walifanikiwa kusawazisha kupitia kwa Boban Zilintusa aliyefunga kwa kichwa baada ya kuruka juu akiwa katikati ya Onyango na Kennedy Juma wakati akimalizia mpira wa faulo uliopigwa na Ibrahim Ahamada dakika ya 46.

Simba ilipoteza nafasi ya bao la mapema baada ya nahodha wake, John Bocco kupiga shuti la kushtukiza pembeni dakika ya kwanza huku Haruna Chanongo naye akiinyima Mtibwa Sugar goli kwa kupiga juu wakati ameshafanya kazi nzuri ya kuwatoka mabeki wa 'Wekundu wa Msimbazi', Kennedy na Onyango dakika ya nne.

Dakika ya saba Bernard Morrison alichelewa kuwahi krosi ndefu iliyopigwa na Shomary Kapombe na kupoteza nafasi ya kufunga akiwa ndani ya eneo la 18 baada ya kudondoka katika harakati za kuuwahi mpira.

Salum Kanoni aliwahi kuutoa nje mpira uliokuwa unamilikiwa na Morrison ambaye alikuwa anaelekea kufunga na kuikosesha Simba bao dakika ya 11 huku kipa Msheri akipangua tena shuti la Clatous Chama sawa na nafasi nyingine iliyotengenezwa na mabingwa hao watetezi iliyopigwa na Bocco dakika 30.

Onyango alikaribia kuifungia Simba, lakini mpira wa kichwa wa dakika ya 42 akiunganisha kona iliyopigwa na Luis Miquissone uligonga mwamba na kutoka nje.

Manula alipangua shuti lililopigwa na Jaffari Kibaya aliyeunganisha pasi ya Salim Kihimbwa na kuwanyima wenyeji nafasi ya kupata bao lingine katika mchezo huo uliochezeshwa na refa, Hamisi Athumani kutoka mkoani Shinyanga, wakati huo ikiwa ni dakika ya 85, huku Geoffrey Luseke akiokoa shuti la Bocco dakika moja baadaye.

Baada ya mechi ya jana, Simba inatarajia kurejea jijini Dar es Salaam kwa ajili ya kujiandaa kuwakaribisha Biashara United ya Musoma katika mchezo wa raundi ya tatu utakaochezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumapili ijayo, ikiwa ni mechi yake ya kwanza nyumbani.

Katika mechi nyingine zilizopigwa jana za ligi hiyo, KMC FC iliendelea kutamba kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu kwa kuibanjua Tanzania Prisons kwa mabao 2-1 mchezo ukipigwa Uwanja wa Uhuru, huku JKT Tanzania ikichezea kichapo cha mabao 2-0 kwenye dimba la Jamhuri jijini Dodoma dhidi ya Dodoma Jiji FC.

# Zlatko, Amri Said ni vita vya rekodi leo

**Na Saada Akida**

WAKATI Yanga ikiikaribisha Mbeya City katika mechi ya Ligi Kuu Bara leo, makocha wa timu hizo, Mserbia Zlatko Krmpotic na Amri Said watakuwa wakiwania rekodi ya kuwa kocha wa kwanza kuiongoza timu yake kuibuka na ushindi tangu wameanza kuziongoza.

Licha ya rekodi ya kuwania kushinda mechi zao za kwanza msimu huu baada ya Yanga kulazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Tanzania Prisons katika mechi ya ufunguzi, huku Mbeya City nayo ikikubali kipigo cha mabao 4-0 kutoka kwa KMC FC, rekodi inayotazamwa zaidi ni ya makocha hao.

Ikumbukwe licha ya Amri kuwapo Mbeya City kuanzia mzunguko wa pili msimu uliopita, lakini timu hizo zilipokutana msimu uliopita zilitoka sare tasa Uwanja wa Mkapa na kisha kufungana 1-1 kwenye dimba la Sokoine jijini Mbeya, hivyo kocha atakayeibuka na ushindi itakuwa ni rekodi nyingine kwake.

Akizungumza na mwandishi wetu jana, Zlatko alisema wapo tayari kwa ajili ya mechi zote zilizo mbele yao, na watapambana kupata pointi tatu kwa kuwa wachezaji wote wapo fiti isipokuwa Balama Mapinduzi ambaye bado ni majeruhi.

"Kikosi kipo vizuri tayari Kwa ajili ya mechi hiyo, tumejiandaa vizuri, wachezaji wanaenda kupambana ili kutafuta pointi tatu, tuna waheshimu wapinzani wetu, kwa sababu nao wamejiandaa kutafuta matokeo chanya," alisema Zlatko.

Kwa upande wa Kocha wa Mbeya City, Amri Said, alisema ana waheshimu Yanga na amewaandaa wachezaji wake kuhakikisha wanatafuta alama tatu za kwanza baada ya kupoteza mechi ya ufunguzi.

"Tumepoteza mechi ya kwanza kwa kufungwa mabao 4-0, nimefanyia kazi makosa yetu na kikosi kipo tayari kupambana kusaka pointi muhimu katika mechi yetu hiyo," alisema Said.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >